Nipashe
Jumatatu Novemba 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581871
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

UKURASA WA 3
**Afariki** dunia akitoka kufanya mtihani, ndugu zake wagoma kuchukua mwili

UKURASA WA 3
**TPA** kuwapunguzia gharama waathirika jengo la Kariakoo


UKURASA WA 5
**Watiwa** mbaroni kwa tuhuma za kupiga mawe treni ya SGR



UKURASA WA 22
ANCELOTTI: MBAPPE HAJAWAHI KUOMBA NAFASI REAL MADRID

# Upandikizaji ini Muhimbili waiva

• **Kati** ya 5,000 wanaohudhuria kliniki ya ini, 2,333 wana uvimbe, 607 wanahitaji kupandikizwa... *Uk. 2*





Rais Samia Suluhu Hassan akitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima katika Uongozi ya Chuo Kikuu Mzumbe na Mkuu wa Chuo hicho, Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein wakati wa mahafali ya 23 ya chuo hicho, mkoani Morogoro jana. Shahada hiyo ni ya kwanza katika ngazi ya uongozi kutolewa na chuo hicho tangu kuanzishwa kwake. **PICHA: IKULU**

## Mbowe: CHADEMA ni mpango wa Mungu, CCM watambia 4R

UKURASA 8



## Rais Samia akiri kuumizwa vurugu za kisiasa Zanzibar

UK. 2

**MICHEZO** RAMOVIC AANIKA UBORA WA AL HILAL UK.24

**MAONI,** UK.6

# Rais Samia akiri kuumizwa vurugu za kisiasa Zanzibar

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa Shahada ya Udaktari wa Heshima ya Uongozi na Chuo Kikuu Mzumbe, huku mwenyewe akikiri kuumizwa na vurugu za kisiasa Zanzibar.

Hiyo ni shahada ya sita ya aina hiyo kwa mkuu wa nchi. Tangu ashike madaraka Machi 19, 2021, ameshatunukiwa shahada zingine tano za udakatri wa heshima katika fani mbalimbali na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. William Mwegoha alisema jana wakati wa mahafali ya 23 kuwa shahada hiyo imetokana na kile alichokifanya Rais Samia madarakani, akiwa kielelezo cha uongozi ndani na nje ya nchi.

Kabla ya shahada hiyo, Rais Samia alitunukiwa shahada zingine na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha India, Chuo Kikuu cha Ankra, Uturuki na Chuo Kikuu cha Anga cha Korea.

Akihutubia wakati wa mahafali hayo jana, mbali na vurugu za kisiasa Zanzibar, Rais Samia alitaja changamoto nyingine alizokabiliana nazo ni pamoja na kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia akiwa madarakani, yeye akiwa makamu wake.

Rais Samia alisema kuwa katika kipindi cha safari yake ya uongozi, vitu ambavyo vimekuwa vikimuumiza ni vurugu za Zanzibar ambazo zilighatimu maisha ya watu.

Alisema kuwa kutokana na vurugu hizo, alishiriki katika kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na sasa wananchi wananufaika na hatua hiyo.

Alisema hatua hiyo ilifikiwa kwa kuzingatia maslahi ya taifa baada ya kufanya utafiti na kupokea ushauri kutoka kwa wadau. Sasa kunashuhudiwa utulivu na amani Zanzibar.

Alisema utawala wake pia ulikumbwa na changamoto nyingine ya janga la UVIKO-19 na vita ya Russia na Ukrane, yote hayo yakileta changamoto ya kuyumba kwa uchumi duniani na kuathiri Tanzania.

**SHAHADA YA HESHIMA**

Kwa mujibu wa Prof. Mwegoha, shahada iliyotolewa jana kwa Rais Samia, ni ya kwanza kutolewa na Chuo Kikuu Mzumbe tangu kuanzishwa kwake. Rais Samia alikuwa mgeni maalumu katika mahafali hayo ya 23 ya chuo hicho mkoani Morogoro.

Mkuu wa Kampasi ya Mzumbe Dar es Salaam, Prof. Cyriacus Binamungu, alisoma wasifu wa Rais Samia na kueleza kwa undani sababu za kumtunuku shahada hiyo.

Alisema kuwa hadi wanafikia uamuzi huo, walipitia kwa umakini katika muktadha wa misingi ya kuanzishwa chuo hicho na kubaini kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia anastahili shahada hiyo.

"Shahada hii ni kielelezo katika kutambua mchango wake (Rais Samia) kwenye jitihada za maendeleo endelevu ya Tanzania na nje ya nchi kwa ujumla," alisema.

Prof. Binamungu alisema Mkuu wa Nchi huyo ameweka historia ya kuwa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke na baadaye kuwa Rais wa kwanza mwanamke nchini.

Katika uongozi wake, alisema Prof. Binamungu kuwa mafanikio mbalimbali yamefikiwa na ndio yanafanya astahili shahada hiyo ya udaktari wa heshima.

Alisema wamezingatia pia uongozi wa Rais Samia tangu akiwa na nafasi nyingine hadi alipokuwa Rais.

Alisema kuwa kwa miaka mitatu ya serikali chini ya Rais Samia, kuna mafanikio katika sekta za elimu, afya, miundombinu, diplomasia, uchumi na demokrasia.

Alisema kuwa ndani ya uongozi wake, Rais Samia ameanzisha falsafa ya 4R iliyojenga msingi wa utawala bora na kuzaa Tume ya Haki Jinai na kikosi kazi.

"Kwa ufupi sana, haya ni baadhi ya mambo yaliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Hatuna shaka kwamba mtunukiwa wetu amejitanabaisha kwamba yale mafunzo anayatumia vema katika kujenga ustawi wa watanzania," alisema Prof. Binamungu.

Kuhusu mahafali, Prof. Mwegoha alisema yamejumuisha wahitimu 5,012. Kati yao, wanawake ni 2,354 na wanaume ni 2,358, karibu asilimia 50 kwa 50.

Pia alisema kuna wahitimu 12 wa shahada ya uzamivu, idadi ambayo ni kubwa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho.

Awali, akitoa salamu za wizara, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alipongeza seneti ya chuo hicho kwa uamuzi wa kikanuni wa kutoa shahada hiyo kwa Rais Samia, huku akimpongeza Mkuu wa Nchi kwa kuwa "anastahili kutokana na uongozi wake wenye maono ya mbali, sahihi na kuwapeleka watu katika njia sahihi".

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus, akikabidhi msaada wa vifaa kinga vya uokozi kwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga (wa tatu kulia), kwa ajili ya kusaidia kazi ya uokoaji yanapotokea majanga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Muhimbili kuanza kupandikiza ini

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) inatarajia kuanza kutoa tiba ya upandikizaji ini mwakani kutokana na kuwapo mahitaji hayo, hasa kwa wagonjwa wanaohudhuria kliniki ya ini hospitalini huko.

Uongozi wa hospitali hiyo ya hadhi ya juu zaidi nchini umesema kuwa zaidi ya wagonjwa 5,000 wana tatizo la ini na kati yao, 2,333 wana uvimbe kwenye ini huku 607 wakigungulika kuwa na saratani ya ini na kusinyaaa kwa ini, hivyo wakihitaji huduma ya kupandikizwa ini.

Mkurugenzi Mtendaji MNH, Prof. Mohamed Janabi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akieleza kuwa kwa mwaka mmoja na nusu, hospitali hiyo imekuwa inafanya maandalizi ya kuanzisha huduma hiyo kwa kushirikiana na matabibu wenzao wa India.

"Kwa hizi siku mbili (mwishoni mwa wiki), tumefanya uchunguzi kwenye OPD (wagonjwa wa nje) na watu wapatao 100 tumewaona, na miongoni mwao tumewakuta wana tatizo. Huu ni mchakato wa kujijengea uwezo, tunahitaji wauguzi, wataalamu wazuri eneo hili.

"Wenzetu wa India wameanza upandikizaji ini tangu mwaka 2002. Kupitia Idara ya Mfumo wa Chakula (ya MNH), walikuwa na wenzetu kutoka India ili mwakani tuanze huduma hii. Tulitaka kujua kwanza wagonjwa wangapi wana tatizo, tumewaona zaidi ya 100. Tunahitaji wataalamu wa usingizi, madaktari, yaani tuwe na seti ya eneo hili," alisema Prof. Janabi.

Alisema kusogeza huduma hizo karibu na wananchi, kutapunguza gharama nyingi za kupeleka wagonjwa hao kutibiwa nje ya nchi. Alisema huduma hizo hazikuwapo nchini kutokana na kukosa utaalamu, vifaa vya uchunguzi au miundombinu stahiki ya kutolea huduma hizo.

"Tumeshirikiana na wataalamu kutoka Hospitali ya Fortis ya India, ambao wamekuwa na madaktari wetu kwa siku tatu, wameona wagonjwa mbalimbali wa magonjwa ya ini na kufanya tathmini ya hali ya upatikanaji dawa, miundombinu ya maabara, ICU (chumba cha uangalizi maalumu) ambayo inakidhi mahitaji ya huduma hiyo," alisema.

Jenifer Choudhary, Mkurugenzi wa Biashara kutoka Vaidam Health ya India, alisema ni furaha kupata fursa ya kufika nchini kwa ajili ya kufanya maandalizi ya huduma hiyo.

"Huduma hii inahitaji kufanya maandalizi na si kufanyika kwa awamu moja pekee na wakati huu tumefika kufanya maandalizi ya awali na kuwafanyia uchunguzi wagonjwa na mahitaji yatakayohitajika ili kufanikisha awamu ya pili.

"Tuna matumaini huduma hii itafanyika kwa uhalisia, lakini awamu za maandalizi zinaweza kufikia tatu kabla ya kuanza upandikizaji kwa wagonjwa," alisema Choudhary.

Dk. Gaurav Gupta kutoka Hospitali ya Fortis ya India, alisema upandikizaji ini ni safari inayohitaji maandalizi na itafanikiwa kutokana na kuwapo vifaa na wataalamu.

Bingwa Mbobezi wa Upasuaji wa Magonjwa ya Mfumo wa Chakula na Ini na Bingwa wa Upasuaji kupitia Tundu Dogo MNH, Dk. Kitembo Salumu alisema kuwa hadi sasa takwimu za hospitali zinaonesha kuna zaidi ya wagonjwa 5,000 wenye shida katika ini.

Alisema kuwa kati yao, 2,333 wana uvimbe kwenye ini na 607 wamegungulika kuwa na tatizo la saratani ya ini, wengine ini kusinyaa na hivyo kuhitaji huduma ya kupandikizwa ini.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

## HABARI KITAIFA

# Afariki dunia akitoka kufanya mtihani, ndugu zake wagoma kuchukua mwili

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mogabiri, wilayani Tarime, mkoani Mara, Julius Nchagwa anadaiwa kufariki dunia baada ya kuanguka katika uwanja wa shule hiyo muda mfupi baada ya kutoka katika chumba cha mtihani.

Ndugu wa mtahiniwa huyo wamegoma kuchukua mwili wake, wakishinikiza uchunguzi kuhusu chanzo cha kifo chake, wakidai miezi kadhaa nyuma alikuwa na ugomvi na uongozi wa shule hiyo.

Mzazi wa mwanafunzi huyo, Daniel Marwa, mkazi wa kijiji cha Nyabitocho, wilayani hapa, alisema hawako tayari kuchukua mwili wa kijana wao kwa kuwa kuna utata juu ya chanzo cha kifo chake.

Alisema hofu ya familia inatokana na madai kwamba miezi kadhaa iliyopita, kijana wao alikuwa na ugomvi na uongozi wa shule hiyo, hali iliyosababisha kusimamishwa masomo na uongozi wa shule.

"Wanafamilia tumeshauriana kwanza tusichukue mwili wa marehemu hadi taratibu zote za uchunguzi zitakapofanyika kwa kuwa kifo cha kijana wetu kina utata kutokana na kuwapo ugomvi baina yake na uongozi wa shule hapo awali," alidai.

Mashuhuda wa tukio hilo walidai mtahiniwa huyo alikuwa anatetemeka, hata kuanguka kwenye uwanja wa mpira na kupoteza fahamu. Inadaiwa alifariki dunia kabla ya kupata huduma za kitabibu.

Mmoja wa wanafunzi shuleni huko, Ng'anga Thomas alidai kuwa yeye na wenzake waliitwa kutoa msaada kwa mtahiniwa akiwa ameanguka kwenye uwanja wa mpira, mita chache kutoka madarasa ya shule hiyo.

"Tulifika eneo hilo na kumkuta akiwa anatetemeka na kuonesha dalili za ajabu ambazo hatukuzielewa wakati huo, tukambeba kumpeleka hospitalini ambako hata hivyo tuliambiwa baadaye alikuwa ameshafariki dunia," alidai mwanafunzi huyo.

**"Wanafamilia tumeshauriana kwanza tusichukue mwili wa marehemu hadi taratibu zote za uchunguzi zitakapofanyika kwa kuwa kifo cha kijana wetu kina utata..."**

Mkuu wa Shule hiyo, Magudila Mgeta alisema mwanafunzi huyo alifanya makosa ya utovu wa nidhamu miezi kadhaa iliyopita ikiwamo kumpiga mwanafunzi mwenzake na kukataa kutii maagizo halali ya walimu.

"Alipelekwa katika Kamati ya Nidhamu, nako pia akakaidi, hatimaye Bodi ya Shule ikaamuru asimamishwe shule, lakini arejee kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, alirejea baadaye shuleni na kuruhusiwa," alisema.

Mwalimu huyo alisema juhudi za kuokoa maisha ya mtahiniwa huyo hazikufanikiwa kwa kuwa alifariki dunia kabla ya kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mji wa Tarime.

Alisema vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi kwa kushirikiana na madaktari ili kuja na maelezo kamili kuhusiana na chanzo cha kifo hicho na kuwa ripoti itakabidhiwa kwa ndugu wa marehemu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA DODOMA
SHAURI LA ARDHI NA. 5552/2024

ANITHA HAULE ........................................MDAI

DHIDI YA

1. DODOMA CITY COUNCIL ........................................MDAIWA
2. THE ATTORNEY GENERAL ........................................MDAIWA
3. THE COMMISSIONER FOR LANDS, MINISTRY OF LANDS,
4. HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT........................................MDAIWA
5. GEOFREY WILLIAM MAUYA ........................................MDAIWA
6. SAMWEL NG'OINA ZAKAYO ........................................MDAIWA

KWA: 1. SAMWEL NG'OINA ZAKAYO
POPOTE PALE ULIPO

YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 5552/2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. **Jaji F. R. Khalfan**, wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu kamili **(9:00)** asubuhi siku ya Jumanne tarehe **26/11/2024.**

**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** hutofika wewe wenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA**; Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe **31** Mwezi wa Octoba, **2024.**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA


# TPA kuwapunguzia gharama waathirika jengo la Kariakoo

**Na Kulwa Mzee**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA) itawapunguzia gharama za uhifadhi mizigo waathirika wa jengo lililoporomoka Kariakoo, jijini Dar es Salaam Novemba 16, mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus, alitoa ahadi hiyo jana kwa waandishi wa habari na kueleza kwamba TPA ina utaratibu wa kuwapunguzia gharama za uhifadhi mizigo waathirika wa majanga ambao ni wateja wa bandari.

Alisema utaratibu wa kuwapa nafuu wadau waliopatwa na majanga pale wanapotoa taarifa zenye mashiko ni wa kawaida na imeshafanya hivyo mara kadhaa kwa utaratibu huu.

"Kuna janga na janga, lipo janga mtu atoondolewa na tozo ya asilimia 50, kuna majanga mengine kulingana na ukubwa, mdau anaweza kuondolewa tozo kabisa.

"Mfanyabiashara atatakiwa kutoa taarifa ya janga lililomkuta kwa wakala wake wa forodha na wakala atawasilisha taarifa hiyo TPA," alisema.

Alieleza kuwa kwa mantiki hiyo, wafanyabiashara na waathirika wa janga la Kariakoo wasiwasiliane na TPA moja kwa moja, bali wawasiliane na mawakala wao.

"Kwa utaratibu wetu tunahifadhi bure mzigo wa mfanyabiashara bandarini kwa siku tano tu baada ya hapo mfanyabiashara atatozwa kodi ya mzigo wake kulingana na siku mzigo huo utakapokaa bandarini," alifafanua.

Pia alisema kuwa TPA inawapa pole wafanyabiashara waliokutwa na tukio hilo, wakiwa kama wadau wakuu wa bandari hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa aliyopewa Rais Samia Suluhu Hassan siku ya Jumatano alipotembelea eneo hilo, watu 20 walikuwa wamepoteza maisha na wengine kadhaa kujeruhiwa na kutibiwa katika hospitali mbalimbali jijini.

Sababu ya kuanguka kwa jengo hilo haijafahamika. Tayari Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa maagizo ya Rais Samia, ameunda kamati maalumu kwa ajili ya ukaguzi wa majengo katika eneo hilo kuu la biashara ili kuepuka maafa katika siku za usoni.

Kamati hiyo pia inachunguza chanzo cha jengo hilo kuporomoka, kukiwa na dokezo kutoka kwa Rais Samia kuwa "hata kwa kuangalia kwa macho, nondo zilizotumika, na ubora wa kuta, vinaonesha ujenzi wa jengo hilo haukusimamiwa vizuri licha ya kupewa vibali na mamlaka husika".

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*


IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM SUB – REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM
CIVIL APPEAL NO. 14747/2024

ALLIANCE INSURANCE CORPORATION LTD ........................APPELANT

VERSUS

MTUNZI SULEIMAN BAMUZY ........................................1ST RESPONDENT
MOHAMED TRANS LIMIUTED ........................................ 2ND RESPONDENT
SAMWEL RAMADHANI SHABAN ........................................3RD RESPONDENT

SUMMONS FOR PUBLICATION

TO:

1. MOHAMED TRANS LIMITED,
2. SAMWEL RAMADHANI SHABAN

**WHEREAS**, the above mentioned case has been fixed for mention on 17th day of December, 2024 at 9:00 A. M before **Hon. H. S. Mtembwa, Judge**. Your are required to appear in this Court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of Court this **31st** day of **October, 2024.**

DEPUTY REGISTRAR

# Kesi watumishi 15 wa jiji ngoma nzito

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi maarufu Mahakama ya Mafisadi, imekataa kupokea kielelezo cha flash yenye taarifa za miamala ya fedha za Manispaa ya Ilala kutokana na shahidi kushindwa kueleza kilichomo ndani yake.

Uamuzi huo wa mahakama umetolewa mbele ya Jaji Sedikia Kisanya wakati shahidi wa tano wa upande wa mashtaka Edgar Paul akitoa ushahidi katika kesi ya kulisababishia jiji hasara ya Sh. bilioni 8.9 inayowakabili watumishi 15.

Washtakiwa katika shauri hilo ni Tulusubya Kamalamo na wenzake 14 wanaokabiliwa na mashtaka 142, yakiwamo ya kuongoza genge la uhalifu, matumizi mabaya ya ofisi na kusababishia jiji hasara ya Sh. bilioni 8.9.

Edgar katika ushahidi wake alidai ni ofisa kutoka Benki ya CRDB na miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha mfumo wa benki unafanya kazi ipasavyo.

Alidai kuwa Machi 12, 2023, akiwa ofisini, alitakiwa kutoa taarifa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhusu miamala ya fedha katika akaunti ya Manispaa ya Ilala kuanzia Januari 2019 hadi Desemba 2021.

"Niliingia katika mfumo wa benki kuchukua taarifa hizo, nilikuta ziko kurasa 10,000, tukaamua kutoa kurasa 10 za mwanzo na kurasa 10 za mwisho kisha taarifa yote ya miamala hiyo nikaingiza katika flash," alidai.

Shahidi aliomba kifaa hicho kipokewe mahakamani kama kielelezo cha upande wa mashtaka.

Upande wa utetezi ulipinga kupokewa kwa kielelezo hicho kwa kuwasilisha hoja mbalimbali.

Wakili Constantine Kakula alidai flash isipokewe kwa sababu shahidi alishindwa kuweka msingi muhimu kwa kuelezea flash na taarifa zilizomo ndani yake.

Alidai shahidi hakueleza anakitambuaje kilichomo ndani ya flash ili atakaporuhusiwa kufungua flash hiyo alichokielezea kikutwe ndani yake.

Hoja nyingine ya upande wa utetezi ni kwamba watuhumiwa hawakupewa nafasi ya kuangalia flash kama kanuni inavyotaka na kwamba wakati wa kusomewa maelezo ya mashahidi, haikutajwa.

Upande wa Jamhuri ulidai wakati washtakiwa wanasomewa maelezo ya mashahidi, flash yenye miamala ya fedha za Manispaa ya Ilala ilisomwa, hivyo hoja hiyo haina mashiko.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Mahakama ilipokea flash kwa ajili ya utambuzi na kukataa kupokewa kama kielelezo cha upande wa mashtaka.

"Shahidi aliomba mahakama kukubali flash yenye taarifa ya benki bila kubainisha vilivyomo ndani yake. Kulingana na hali ilivyo, mahakama inaona kwamba shahidi alishindwa kuonesha flash disk na taarifa zilizomo ndani yake kama inavyotakiwa na sheria.

"Kwa tukio hili, ninaunga mkono hoja ya pingamizi flash inayoombwa kupokewa kama kielelezo, hairuhusiwi kupokewa," alisema Jaji Kisanya.

Mahakama hiyo ilikubaliana na hoja moja ya Wakili Kakula kwamba shahidi alishindwa kuelezea kilichomo ndani ya flash.

Washtakiwa katika shauri hilo wanadaiwa kati ya mwaka 2019 na mwaka 2021, waliongoza genge la uhalifu, matumizi mabaya ya madaraka kwa kushindwa kuingiza mapato ya Halmashauri ya Jiji yanayotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato katika akaunti za CRDB, NMB, NBC na DCB na hivyo kujipatia manufaa ya Sh. bilioni 8.9.

Pia wanadaiwa kulisababishia Jiji la Ilala hasara ya kiasi hicho cha fedha. Shauri hilo linaendelea leo.



Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Charles Mwamaja, akikagua samani zilizoko katika ukumbi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini alipotembelea kabla ya kufanyika mahafali ya 38 yaliyofanyika Dodoma jana. Kulia aliyeshika kipaza sauti ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Hozen Mayaya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Lori ladaiwa kunaswa likiwa na shehena dawa feki za mifugo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wawili, akiwamo mfanyabiashara wa dawa za mifugo Nickson James (29), mkazi wa mtaa wa Buswelo, Manispaa ya Ilemela, mkoani Mwanza, wakidaiwa kukamatwa wakati wanasafirisha dawa za mifugo zinazodhaniwa ni bandia zenye thamani ya Sh. 78,986,099.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa kutokana na operesheni zinazoendelea katika maeneo yote ya mkoa huo, Novemba 7 mwaka huu, saa 6:30 mchana, huko katika kijiji cha Lilondo, kata ya Wino, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, askari polisi walikamata gari lenye namba za usagili T 185 EBX aina ya Toyota DYNA Truck ambalo lilikuwa linaendeshwa na Frank Ndunguru.

Alidai kuwa gari hilo lilikuwa linatoka Songea kwenda Njombe likiwa limesheheni dawa za mifugo na kwamba mfanyabiashara James aliyekuwa katika gari hilo, ndiye mmiliki wa dawa hizo zilizokamatwa, zikihifadhiwa katika gari lenye kiyoyozi (air conditioner).

Hata hivyo, alidai kuwa ukaguzi wa polisi ulibaini air conditioner hiyo ilikuwa feki.

Kamanda Chilya alifafanua zaidi kuwa baada ya gari hilo kukamatwa, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na timu ya wataalamu wa ukaguzi wa dawa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) walibaini dawa hizo zimeingizwa nchini kinyume cha sheria kupitia njia za panya na kwamba baadhi ya dawa ni bandia na nyingine zipo chini ya kiwango kwa mchanganuo:

Levimox Super, Alben Blue, Oxysol Plus, Bisol, Piperazine, Tylodoxy200 na Vetoxy 20 kati yake zikiwa chupa 4,044, madumu 1,646 na pakiti 46 zenye thamani ya Sh. 51,174,599; dawa bandia za mifugo aina ya 03 ambazo ni Hi-tet, Levafas Diamond Naoxy-met 10 inj 500ml & 250mlkati yake zikiwa chupa 1,026, madumu 12 zenye thamani ya Sh. 19,456,000; dawa zilizosajiliwa lakini hazina kibali cha kuingia nchini aina ya 03 ambazo ni Ivermed Ascarex na Polytricin kati yake zikiwa chupa 512, pakiti 92 zenye thamani ya Sh. 8,355,500.

Kamanda Chilya alisema upelelezi wa kina juu ya tukio hilo unaendelea kwa kushirikiana na mamlaka husika na jalada la kesi limefikishwa Ofisi ya Mashtaka mkoani Ruvuma kwa hatua zaidi za kisheria.

# Wivu wa wapenzi wasababisha vifo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATU wawili wamefariki dunia katika matukio tofauti, likiwamo la mwanamke Marcelina Chigudulu aliyekutwa amefariki dunia chooni katika chumba alimokuwa amepanga na mwenza wake ndani ya nyumba ya kulala wageni 'Maleta Lodge', kijijini Kilosa, nje kidogo ya Mji wa Mbambabay, wilayani Nyasa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya alisema mwishoni mwa wiki kuwa, Novemba 17 mwaka huu, saa tatu usiku, katika nyumba hiyo ya kulala wageni, Marcelina, aliyekuwa na ujauzito wa miezi mitatu, alikutwa amefariki dunia.

Kamanda Chilya alisema kwamba inadaiwa siku hiyo ya tukio, Marcelina aliingia katika nyumba hiyo akiwa na mpenzi wake, Hassani Kamtande ambaye ni fundi magari, mkazi wa kijiji cha Buluma, wilayani Mbinga. Ilipotimu saa tatu usiku, iligundulika chumba alimokuwa Marcelina, kinawaka moto, kitendo ambacho kilisababisha majirani kufika eneo hilo kusaidia kuzima moto.

Alisema wakati majirani wakiwa wanaendelea na uzimaji moto katika chumba hicho, waligundua kuwamo mwili wa binadamu uliokuwa umelazwa chooni wakati mwenza wa Marcelina akiwa hayumo katika chumba hicho, akidaiwa kukimbia baada ya kufanya mauaji.

Alieleza kuwa baada ya upelelezi wa kina wa tukio hilo, Jeshi la Polisi lilibaini mtuhumiwa alikuwa na wivu wa mapenzi kwa mwenza wake na ndicho kiini cha kumnyonga wakiwa ndani ya chumba hicho cha kulala wageni na kuchoma vitu mbalimbali likiwamo godoro kwa lengo la kupoteza ushahidi.

Kamanda Chilya alisema mtuhumiwa wa tukio hilo, Kamtande ameshakamatwa na anatarajiwa kufikishwa mahakamani kwa hatua zaidi ya kisheria.

Katika tukio lingine, Kamanda wa Chilya alisema ni la Novemba 14 mwaka huu, saa 12 asubuhi, kitongoji cha Mbilo, kijiji cha Kizuka, tarafa ya Muhukuru, wilayani Songea, ambako Ponsiana Kapinga (22), mkazi wa kitongoji hicho, aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na mumewe Martini Hyera baada ya kumnyima tendo la ndoa kwa muda mrefu.

Alisema kuwa wawili hao walionekana alfajiri wakikimbizana huku mtuhumiwa akiwa ameshika mpini wa shoka na baadaye kutekeleza mauaji hayo kisha kumpigia simu shangazi yake Paulina Nchimbi na kumjulisha kuwa amemuua mke wake na akataja sababu za kumuua kuwa alikuwa anamnyima unyumba kwa muda mrefu.

Kamanda Chilya alisema mwili wa Ponsiana umefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi. Mtuhumiwa Hyera baada ya tukio hilo alikimbia na kutokomea kusikojulikana. Msako dhidi yake unaendelea.

# Watiwa mbaroni tuhuma za kupiga mawe treni ya SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi linawashikilia watoto wawili kwa tuhuma za kurusha mawe na kuharibu kwa kuvunja vioo viwili vya treni ya mwendokasi (SGR) katika Kijiji cha Manase, wilayani Chamwino.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, DCP David Misime, watoto hao walirusha mawe wakati treni hiyo inapita ikitokea jijini Dar es Salaam kwenda jijini Dodoma Novemba 22, mwaka huu.

Alisema kutokana na hali hiyo, polisi walifanya msako na kuwakamata watoto hao wenye umri wa miaka 16 na 12 (majina tunahifadhi kwa sababu watuhumiwa ni watoto na wanalindwa kisheria), wote wakazi wa kijiji cha Manase wilayani Chamwino.

"Chanzo kilichosababisha uharibifu huo ni baada ya kuona treni ikipita, wakarusha mawe kwa pamoja ili kuona kama mawe waliyorusha yataweza kushindana na mwendo wa treni," alisema.

DCP Misime alitoa wito kwa wananchi wanaoishi maeneo ambamo treni ya kisasa inapita, kuendelea kupeana elimu juu ya umuhimu wa kulinda miundombinu ya treni kwa maslahi yao na taifa.

"Kila mzazi au mlezi anao wajibu wa kutoa elimu kwa familia, hasa watoto kuacha vitendo ambavyo vitasababisha uharibifu kwa reli na treni ya kisasa kwa kuwa itawasababishia kukinzana na sheria za nchi," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Uongozi wa chuo waiangukia serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHUO cha Maendeleo ya wananchi Kibaha kinakabiliwa na vikwazo mbalimbali, ukiwamo uhaba wa karakana kwa ajili ya fani za umeme, useremala na ufundi wa ujenzi wa mabomba.

Pia kinahitaji gari la usafiri na usafirishaji huku baadhi ya majengo yakiwa na uhitaji wa ukarabati.

Mkuu wa chuo hicho , Joseph Nchimbi alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali yaliyofanyika chuoni huko kwa wahitimu 147 wa fani mbalimbali, akiomba serikali kusaidia fedha za ukarabati na ujenzi wa majengo mapya.

Nchimbi pia aliomba serikali kusaidia fedha za ruzuku kwa ajili ya chakula na uendeshaji wa chuo hicho kama ilivyo kwa vyuo vingine vya FDC vilivyo chini ya Wizara ya Elimu.

Alibainisha kikwazo kingine ni baadhi ya wanachuo kukatisha mafunzo kabla ya kuhitimu muda uliopangwa baada ya kuona wametosheka au kushindwa kumudu gharama za chakula.

"Chuo hiki kinategemea ada, michango ya wazazi kujiendesha hakipati ruzuku ya serikali kwa ajili ya chakula na mahitaji mengine ya uendeshaji kama ilivyo kwa vyuo vingine vya FDC na hivyo kufanya kishindwe kutoa chakula," alisema Nchimbi. Mkurugenzi wa Elimu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Emmanuel Shindika, akizungumza katika mahafali hayo alisema serikali itaendelea kupeleka fedha za ukarabati wa mabweni ya wanachuo na miundombinu mingine, huku akiahidi serikali itaangalia namna ya kutatua changamoto zingine zilizoko.

Alisema serikali imejipambanua katika kuimarisha uchumi kwa kuwa na sera nzuri za kibenki, ukopeshaji na ushirika wa akiba na mikopo na hivyo vijana wanaohitimu wanatakiwa kutumia fursa hizo kwa kujiunga kwenye vikundi na kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri.

Pia aliwataka wahitimu wa chuo hicho kujiunga na vikundi vya uzalishaji mali ambavyo vitakuwa njia ya mafanikio itakayopapatia fursa ya kuunganisha ujuzi na kutumia rasilimali zitakazopatikana katika maeneo yao.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Robert Shilingi, aliomba serikali kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya chuo hicho ili vijana wanaojiunga katika chuo hicho wasome katika mazingira mazuri.

# Tanzania, Uganda kushirikiana katika miradi ya mafuta na gesi

**Na Frank Monyo**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio amesema Tanzania na Uganda zitaendelea kushirikiana katika uendelezaji miradi mbalimbali ya nishati, ikiwamo sekta ya mafuta na gesi.

Dk. Mataragio aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kushiriki Jukwaa la Kibiashara kati ya Tanzania na Uganda.

"Tunaangalia ni kwa jinsi gani sekta hii ya mafuta na gesi inaweza ikachangia katika maendeleo ya nchi hizi mbili, tumekuwa na mijadala mbalimbali inayolenga kuendeleza sekta hii ya mafuta na gesi," alisema Dk. Mataragio.

Aliongeza kuwa, mjadala mkubwa katika jukwaa hilo ni kuangalia namna gani nchi za Tanzania na Uganda zinaweza kushirikiana katika sekta za mafuta na gesi.

Mataragio alisema Tanzania na Uganda zina historia ndefu za ushirikiano, akitolea mfano mradi wa kimkakati wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi wa EACOP.

Akielezea mradi huo wa EACOP, Dk. Mataragio alisema umefikia asilimia 47, akisisitiza kuwa kwa sasa uko katika hatua ya kutandaza mabomba. Takribani kilomita 52 za mabomba zimeshachomelewa ambazo zitaanza kufukiwa ardhini.

Akizungumzia faida ya mradi kwa wananchi, alisema Watanzania wamejengewa uwezo katika maeneo mbalimbali na hivi sasa wanafanya kazi kwenye mradi huo.

Kwa upande wa ajira, alisema mradi umetoa zaidi ya ajira 8,000 huku lengo likiwa ajira 10,000.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI MKUTANO WA PILI WA JUMUIYA YA WAHASIBU WAKUU WA SERIKALI AFRIKA-AAAG

Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wahasibu wa Serikali wa Afrika mwaka 2024 (AAAG) utakaofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba, 2024.

Mkutano wa pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Serikali Afrika utakuwa na mada mtambuka ambazo zitasaidia watumishi wa kada mbalimbali kuwaongezea ujuzi na Maarifa.

Pia Mkutano huu utasaidia Viongozi na Watumishi wa Tanzania kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na kupeana fursa na Viongozi na Watumishi toka nchi nyingine za Afrika, Benki ya Dunia na IMF. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ada ya ushiriki ya mkutano ni **Shilingi za Kitanzania 1,300,000/=** kwa kila mshiriki. Hivyo, Mamlaka husika zinaombwa kuwaruhusu na kuwalipia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Maafisa Usimamizi wa Fedha, Maafisa TEHAMA na watumishi wa kada nyingine kuhudhuria mkutano huu.

Washiriki wote wanatakiwa kuanza kijisajili kupitia lango (portal) lifuatalo: https://conference.aaag.org.zm kuanzia sasa hadi tarehe 01 Disemba, 2024 na ada ya ushiriki ilipwe kupitia **akaunti namba 9924915301 yenye jina African Association of Accountants General (AAAG).**

Aidha, kwa Taasisi za Umma, Kampuni mbalimbali na watu binafsi wanaotaka kudhamini Mkutano huu kwa lengo la kujitangaza kibiashara na kufanikisha Mkutano huu; Wizara ya Fedha inawakaribisha.

Kwa mawasiliano zaidi piga Namba ya simu +255 713 525 592 barua pepe, veronica.kishala@hazina.go.tz na evans.sayile@hazina.go.tz Sanduku la Posta ni Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha S.L.P 2802, Dodoma.

Pia kama muombaji amesahau namba ya simu, barua pepe na Sanduku la Posta anaweza kupata mawasiliano kupitia wakuu wa Hazina Ndogo waliopo kila mkoa Tanzania bara na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**

**Sekretariati ya Kamati ya Maandalizi Mkutano wa AAAG,**
**Wizara ya Fedha**
**Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Novemba, 2024**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Simba, Yanga shindeni mechi zenu za kwanza nyumbani

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga na Simba, kesho na keshokutwa watashuka dimbani katika michezo yao ya kwanza hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, kesho watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza na mabingwa wa Sudan, Al Hilal Omdurman, katika mchezo wa raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

Kesho kutwa, Simba nayo itakuwa kwenye uwanja huo huo kucheza mchezo wake wa kwanza, hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola.

Katika hatua hii, lengo namba moja kwa timu zote ni kutinga hatua ya robo fainali, hivyo kama zinataka kufika huko zinapaswa kushinda michezo yao hiyo ya kwanza ili kuongeza ari ya upambanaji.

Kwa bahati nzuri timu zote zinacheza nyumbani, hivyo tunatarajiwa zitatumia vema faida ya kucheza nyumbani ili kupata ushindi, ikiwezekana mnono.

Tunajua hatua hizi za makundi timu nyingi kufanya kila mbinu kuhakikisha zinashinda kwenye viwanja vyao vya nyumbani na zikienda ugenini hulazimisha angalau sare. Hivyo ili kufika robo fainali kwenye michuano hii Simba na Yanga zinatakiwa ziwe na utamaduni wa kushinda mechi zake nyumbani.

Mahesabu ya hatua hizi za makundi ni kwamba timu inayoshinda mechi zake tatu za nyumbani kwa ushindi mnono, hata kama ikipoteza zile za ugenini ina uwezekano mkubwa wa kuvuka na kwenda robo fainali, kama ilivyofanya Simba, 2019 Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo pamoja na kupoteza michezo yake yote mitatu ugenini, tena ilichapwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Al Ahly ya Misri, lakini ushindi wa mabao machache tu kwenye michezo ya nyumbani uliifanya kushika nafasi ya pili nyuma ya Wamisri hao.

Huu ni wakati wa wachezaji kujituma, kwani michuano hii hutazamwa na klabu nyingi Afrika na nje ya bara hili. Kujituma kwao, kupambana kwa ajili ya timu, kutawafanya pia kujiwekea mazingira mazuri ya kujipandisha thamani, hivyo kununuliliwa na klabu kubwa zaidi ndani na nje ya Afrika.

Luis Miquissone alionekana wakati akiichezea Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika 2021, alipoifunga Al Ahly na wakaamua kuondoka naye na hilo liliwahi pia kutokea 2011, Mbwana Samatta alipokuwa akiichezea Simba kwenye mechi dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, wakaondoka naye kwa dau kubwa.

Kifupi hii ndiyo michuano ya kujiuza, kama ambavyo Fiston Mayele wa Yanga walipocheza Kombe la Shirikisho misimu miwili iliyopita alionekana na Pyramids.


Lakini pia, katika kaufanikisha hilo, tunawaomba mashabiki wa Simba na Yanga kujitokeza kwa wingi uwanjani kwa ajili ya kuzipa sapoti timu zao kwani siku zote shabiki ni mchezaji wa 12.

Katika hilo, Kocha Pitso Mosimane wakati huo akiwa Al Ahly, aliwahi kukiri kuwa mara nyingi wanapokuja kucheza hapa nchini, hasa na Simba hufikiria zaidi mashabiki wanaojazana uwanjani na kushangilia kwa nguvu, jambo ambalo lilikuwa likiwavuruga.

Akiwa anaziasa timu zinapokwenda kucheza Benjamin Mkapa, kujiandaa kisaikolojia. Hivyo hii ni sifa kubwa kwa Watanzania na hawatakiwi kuiacha. Japo bado hawajakuwa na utamaduni wa kushangilia kwa muda wote wa dakika 90 kwa nguvu ile ile, lakini angalau kwa hiki walichojaliwa nacho wanapaswa kujazana uwanjani kesho na keshokutwa kuzipa sapoti Yanga na Simba.

Sisi tunazitakia kila la kheri timu zote mbili ambazo ni nembo ya soka la Tanzania ili zipate ushindi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mgeni rasmi kila mechi Ligi Kuu Bara sasa kumepitwa na wakati

Na Adam Fungamwango

**ZAMANI** waliitwa wageni wa heshima, siku hizi wanaitwa wageni rasmi. Ni watu au viongozi wanaokuja uwanjani kwa ajili ya sababu maalum, ikiwamo kutoa zawadi na kukabidhi kombe.

Huu ni utamaduni wa tangu miaka ya nyuma, lakini ukiangalia kwa wenzetu ambao walioanzisha soka wameshaachana na hayo.

Ukiangalia ligi mbalimbali duniani Ulaya na Afrika, huwezi kukuta kuna mgeni rasmi kwa mechi kama ya ligi isikuwa ya kukabidhiwa kombe. Utawaona kwenye michuano kama fainali za AFCON, kufungua mashindano na kufunga. Hata Ulaya ni hivyo hivyo. Kwa sasa huwezi kuwaona wageni rasmi kwenye kila mchezo.

Hapa Tanzania utamaduni huo umeonekana kuendelea kwa kile kinachoonekana ni mazoea.

Kila mchezo uwe ni wa Ligi Kuu au Championship, basi utamwona mgeni rasmi, tena yoyote yule, ili mradi tu inawezekana mtu kidogo mwenye wadhifa wake kwenye taasisi, serikalini au chama cha soka.

Binafsi, naona kama utamaduni huu umepitwa na wakati, badala yake waache soka liendelee kuwa soka na mgeni rasmi awepo kwenye mashindano au matukio makubwa.

Kinachotakiwa hapa ni kwamba hata siku mashabiki wakisikia mgeni rasmi, kwenye mechi kubwa na muhimu na mara nyingi wanakuwa ni viongozi wakubwa basi wawe na hamu ya kuona tukio hilo, tofauti na sasa ambapo wageni rasmi wamekuwa wengi.

Kitendo cha kila mchezo kuwa na mgeni rasmi ambaye anaingia uwanjani kupiga picha na wachezaji pamoja na waamuzi wakati mwingine ndiko kunakosababisha baadhi ya wanasiasa kujiingiza moja kwa moja kwenye masuala ya soka ambapo Shirikisho la Mpira wa Miguu Dunia (FIFA), wameshakataa.

FIFA wameshafanikiwa kwa kiasi kikubwa kutenganisha vitu hivyo, pamoja hata na kuwaengua askari polisi kulinda usalama ndani ya uwanja.

Ukiangalia askari kwa sasa kwenye michezo ya kimataifa wanalinda zaidi nje ya uwanja na ndani kuna watu maalum tu walioandaliwa na kupewa mafunzo kwa ajili hiyo.

FIFA na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wanaona mashabiki wanaokuwa uwanjani si wahalifu, bali ni wateja wao, hivyo hawahitaji nguvu iliyopitiliza, badala yake yeyote anayekwenda kinyume cha utaratibu, walinzi maalum wanajua jinsi gani ya kudili naye kwa namna ambayo wamefundishwa.

Mfano wa hili ni wale mabaunsa wa Al Ahli Tripoli ambao walikuwa wanawalinda wachezaji wa timu hiyo waliokuwa wakihofia kufanyiwa vurugu na mashabiki wa Simba kulipa kisasi cha kile kilichotokea Libya, walizuiwa kuingia uwanjani. Kwanza hawakuwa na tiketi, pili hawakutakiwa kwa sababu ya kutoleta taharuki na kuambiwa hata ndani ya uwanja kuna walinzi ambao watawalinda wachezaji hao na si wao. Na hii ni kwa sababu ilikuwa ni michuano inayosimamiwa na CAF. Sijui kama ingekuwa ni ligi ingekuwaje kama wangeingia nao uwanjani au vipi.

Hii inaonesha kuwa wenzetu, wamekuwa wakipiga hatua kila miaka inavyozidi kusonga mbele si kwenye maendeleo ya soka na miundombinu tu, lakini hata kwa maeneo mbalimbali, ikiwamo ulinzi, itifaki na vingine vinavyofanana na hivyo.

Ndiyo maana tunaona leo hawana mgeni rasmi, hadi pale kwenye ufunguzi wa michuano mikubwa na mechi ya fainali na wanaokwenda hapo ni viongozi wakubwa wa nchi na mashirikisho ya michezo.

Hapa kwetu hadi leo, mjumbe wa chama cha soka anakuwa mgeni rasmi wa mchezo. Shabiki akiruka kutaka kuingia uwanjani anakimbiliwa na askari na kupigwa virungu kama mwizi aliyepora simu.

Nadhani umefika wakati tuangalie wenzetu wanafanyaje, ili na sisi twende kutokana na mabadiliko. Isije tukawa tunakwenda sehemu ambayo wenzetu wanatoka.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA: UHANDISI, UNUNUZI, UJENZI NA UZINDUZI WA MUUNDOMBINU WA CHINI WA MHIMILI MMOJA WA UMEME WA JUA WA 3MWP KWA AJILI YA MATUMIZI BINAFSI YA KITUO CHA BAHARINI CHA EACOP MKOANI TANGA. KUMBUKUMBU NA.: 00000669

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya Uhandisi,Ununuzi, Ujenzi na Uzinduzi wa Muundombinu wa chini Umeme wa Jua wa 3MWp wenye Mhimili mmoja kwa ajili ya matumizi binafsi ya Kituo cha Baharini cha EACOP mkoani Tanga.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA KAZI**

**1. Mawanda ya Uhandisi, Ununuzi, Ujenzi na Uzinduzi**

a. **Usimamizi wa Mradi:** Usimamizi wa ujumla ili kutumiza masharti ya mkataba na kukamilisha kazi, ikiwa ni pamoja na :- Usimamizi wa Mradi, Usimamizi wa Ubora, - na Usimamizi wa Afya, Usalama na Mazingira (HSE).

b. **Uhandisi na Uhifadhi wa Nyaraka:** Pamoja na mambo mengine kazi ya Usanifu na Uhandisi itajumuisha nyaraka zifuatazo kama zinavyohitajika katika kujenga na kulinda Mradi kwa ukamilifu: - Nyaraka za Uhandisi na Usanifu - Nyaraka za manunuzi na Ujenzi – Vyeti – Nyaraka za Majaribio ya Kukubalika kwa Kiwanda – Nyaraka ya ukamilifu wa Mitambo – Nyaraka za Uzinduzi na Majaribio.

c. **Manununuzi: Ugavi wa vifaa vyote vipya, vilivyo kamilika, visivyo na kasoro, na visivyokuwa na matatizo:** - Muundombinu wa umeme wa jua (PV) - Muundombinu wa unyenyuaji wa paneli za mfumo wa umeme wa jua– vifuatiliaji – Uzio na geti – vituo vya Hali vya Hewa -mfumo wa Umeme – Mfumo wa Ufuatiliaji na Udhibiti - Vipuli.

d. **Ujenzi na Usimikaji:** inajumuisha rasilimali zote, zana, vifaa, na watendakazi ili kuwa na ujenzi sahihi, usanikishaji na majaribio ya Mradi: Utoaji ishara, ulinzi, taa, uzingatiaji vifaa vya Huduma ya Kwanza – Kazi za Ujenzi – Ufundi mitambo, – Kazi za Umeme – Uzinduzi na majaribio, Uhusiano wa Uunganishaji wa kazi – Upakuaji, usafirishaji na upakuaji, uhifadhi katika eneo la kazi– Kazi – Usafishaji na Udhibiti – Matengenzo kablla ya Kukubalika rasmi kwa Mradi.

**2. Mawanda ya Uendeshajina Matengenezo (O&M)**

Huduma bora ya O&M: kwa miaka miwili ya mwanzo baada ya uzinduzi, kampuni itakuwa na haki ya kusitisha huduma baada ya mwisho wa mwaka wa pili. – Huduma ya Hiari ya O&Q: Kippindi cha kwanza cha miaka 20 kina uwezekanao wa kusitisha huduma pale inapofaa ndani ya miaka 2,5,10 au 15.

**VIGEZO MUHIMU:**

**Kampuni au taasisi zinzoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu na uwezo wa kutoa huduma katika mawanda yanayohitajika Maelezo ya kina ya shughuli au miradi iliyofanyika inayofanana na huu wa (3MVp) kuonesha ushahidi timu iliyopo inayostahili na yenye uelewa wa maeneo ya bomba la mafuta, na rekodii ya thabiti ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Cheti cha usajili na ripoti ya sasa ya ukaguzi wa BRELA (Ambatanisha nakala).
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Leseni ya biashara.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii (Cheti cha ISO 9001, Cheti cha ISO 14001, na OHSAS 18001).
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu.
- Pale inapofaa, uthibitisho wa usajili wa bodi ya kitaaluma, kwa mfano Bodi ya Usajili ya Wahandisi, au Bodi ya Usajili ya Wakandarasi.

Kampuni au taasisi zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya **tarehe** 21 **Disemba 2024**. Kichwa cha Barua pepe kiw e **00000669 – Uhandisi,Ununuzi, Ujenzi na Uzinduzi wa Muundombinu wa chini wa Mhimili mmoj a**
**wa Umeme wa Jua wa 3MWp kwa ajili ya matumizi binafsi ya Kituo cha Baharini cha EACOP mkoani Tanga.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa kumi (10) hadi ishirini (20). **Maombo yote ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingeresa.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya kampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Kampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni ya awali yenye vigezo baada ya kampuni hlyo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA: UTOAJI HUDUMA YA MAJENERATA YA MUDA/ VIFAA VYA KUKUZA NA KUSAMBAZIA UMEME PAMOJA NA VIPURI VYAKE KUMBUKUMBU NA. REQ-00000648

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya Majenerata ya muda/ Vifaa vya kukuza na kusambazia umeme Pamoja na vipuri vyake kwa ajili ya Mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA KAZI**

Ikiwa ni sehemu ya shughuli za Kampuni za ujenzi katika maeneo yake yote ya mradi ndani ya mikoa minane iliyopitiwa na Bomba la EACOP nchini Tanzania, EACOP inatafuta kampuni au mashirika yenye sifa na uwezo wa kutoa huduma ya majenereta ya muda/ Vifaa vya kukuza na kusambazia umeme Pamoja na vipuri vyake kwa kipindi cha hadi miezi 22. Mahitaji ya vifaa na huduma yatajumuisha:

- Utoaji wa majenereta 14 ya muda yenye ukubwa wa kati ya 75kVA na 1.5MVA ikijumuisha kifaa cha usambazaji, nyaya na vipuri.
- Utoaji wa Vifaa vya kukuza na kusambazia umeme vya takribani 5 DC vya ukubwa UPS ulio kati ya kVA 10 na kVA 150.
- Mtoa huduma aliyechaguliwa atawajibika kwa uhamasishaji, ufungaji na uondoaji wa majenereta ya muda ya umeme, Vifaa vya kukuza na kusambazia umeme, ufungaji wa nyaya, vifaa vya usambazaji na viambatanisho vyake.
- Mtoa huduma aliyechaguliwa atawajibika kwa huduma na matengenezo ya majenereta ya muda ya umeme.
- Vifaa vya muda vitahitajika katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania kando ya mkuza wa bomba ili kuendana na mpangilio wa shughuli za uzinduzi.
- Vifaa vyote vilivyotolewa vitadhibitishwa na kukaguliwa kulingana na viwango vya kitaifa na vya mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**

**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**

- Maelezo mafupi yanayoonesha uzoefu, utalaam na uwezo wa kutoa huduma kama hiyo.
- Maelezo ya miradi au shughuli zinazofanana au zilizozofanywa zinazotoa uthibitisho wa timu iliyopo yenye uwezo, ujuzi na ufahamu na uzoefu wa maeneo ya ya bomba na uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA na leseni ya Biashara (Ambatanisha nakala).
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Sera YA Haki za Binandamu.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya **tarehe 27 Disemba 2024** . Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000648 – Utoaji Huduma ya Majenerata ya muda/ Vifaa vya kpima na kukuza umeme Pamoja na vipuli vyake (TZ). Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.** Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakayojumuishwa kwenye orodha ya (Kampuni) ya awali iliyokidhi vigezo. Kampuni ziliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo zitakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA (COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM COMMERCIAL CASE NO 9164/2024**
**BETWEEN**

**LAKE PIPES LIMITED........... PLAINTIFF VERSUS**
**PLANCON (T) LIMITED.........DEFENDANT**

**DEC REE**

**WHERE AS** the plaintiff prays for the judgment, decree and orders against the Defendant as follows:-

1. That the Honourable Court be pleased to order that the Defendant is in (continuous) breach and default of the agreement for supply of construction finishing goods, to wit, HDPE Pipes class C and D.

2. That the Honourable Court be pleased to order the Defendant to pay the Plaintiff TZS 96,005,283.91/= (Tanzania Shillings Ninety-Six Million, Five Thousand, Two Hundred Eighty-Three and Ninety-One Cents) being the outstanding purchase price for the HDPE Pipes supplied to the Defendant by the Plaintiff.

3. That the Honourable Court be pleased to order the Defendant to pay the Plaintiff interest on the decretal sum at the commercial rate of 19% per annum from the date of the breach to the date of delivery of the judgement.

4. That the Honourable Court be pleased to order the Defendant to pay the Plaintiff interest on the decretal amount at the court's rate of 12% per annum from the date of judgment to the date of full and final satisfaction.

5. General damages as will be assessed by this Court.

6. Costs of the suit

7. Any other relief as the Court may find just, convenient, and equitable to grant.

This case coming for judgment on this 15th day of November 2024 in the presence of Ms Beatha Telly, Advocate for the Plaintiff.

**T HIS COURT DOTH HEREBY ORD ER THAT:**

Default judgment is entered in favour of the plaintiff and the following reliefs are granted:-

i. It is hereby declared that the Defendant is in continuous breach and default of the agreement for supply of construction finishing goods, to wit, HDPE Pipes class C and D.

ii. The Defendant is hereby ordered to pay the Plaintiff TZS 96,005,283.91/= (Tanzania Shillings Ninety-Six Million and Five Thousand, Two Hundred Eighty-Three and Ninety-One Cents only) being the outstanding purchase price for the HDPE Pipes supplied to the Defendant by the Plaintiff.

iii. The Defendant is hereby ordered to pay the Plaintiff interest on the decretal sum at the commercial rate of 19% per annum from the date of delivery of the second consignment of goods on 11th May 2023 to the date of delivery of judgement.

iv. The Defendant is hereby ordered to pay the Plaintiff interest on the decretal sum at the court's rate of 7% per annum from the date of judgment to the date of full and final satisfaction thereof.

v. The Defendant is hereby ordered to pay the Plaintiff general damages at the tune of TZS 15,000,000/= for inconveniences suffered.

I further Order that the decree emanating from this suit shall not be executed unless the decree holder has complied with the provisions of Rule 22 (2) (a) and (b) High Court (Commercial Division) Procedure Rules, 2012 (as amended, in 2019). It is so ordered.

Given under my hand and the Seal of the Court this 15th day of November, 2024.

**A.H.GONZI**
**JUDGE**
**15/11/2024**

# Mbowe: CHADEMA ni mpango wa Mungu, CCM watambia 4R

**Na Waandishi Wetu**

KAMPENI za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zinaendelea. Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema chama hicho ni "mpango wa Mungu" ndiyo maana licha ya vikwazo vingi kimeendelea kuwa imara.

Wakati Mbowe anatoa kauli hiyo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimesema uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan umewafilisi hoja zote wapinzani kwa sababu yote yaliyokuwa yanapigiwa kelele ameyatekeleza.

Chama hicho kinachoongoza serikali kimesema Falsafa ya R4 (Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuiding (Kujenga upya) ya Rais Samia ni mtaji mkubwa kwao.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa chama hicho, Amos Makalla, aliyasema hayo jana wakati wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Kata ya Kivule, Jimbo la Ukonga, Dar es Salaam, ikiwa ni siku ya tano ya kampeni mkoani humo. "Wamekubali kuwa muziki huu CCM wanayo haki kupita kwa kishindo. Siasa si ugomvi. Na huyu wa Chama cha TLP (Mwenyekiti wa TLP, Aivan Maganza) ameona namna serikali na uongozi wa Rais Samia kazi alizofanya.

"Kwa kweli Rais Samia amewafilisi hoja zote wapinzani, yote yaliyokuwa yakipigiwa kelele ameyafanyia kazi," alitamba Makalla ambaye pia ni Mlezi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam.

Makalla alisema yanayoendelea mikoani, kwa lugha nyepesi kwa CCM ni kwamba 'yajayo yanafurahisha' akifafanua kuwa ushindi wa kishindo kwa chama tawala unakuja.

Aliwaomba wananchi wawachague wasaidizi wazuri wa mitaa kutoka chama tawala kwa kuwa mafanikio yote ni ushirikiano kati ya viongozi wa chini hadi ngazi ya Rais.

**'MPANGO WA MUNGU'**

Wakati CCM wakitamba na R4, Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe, amesema kuwa baada ya chama hicho kupita katika kile anachokiita "bonde la uvuli wa umauti" kwa miaka saba, wamejipanga kurejesha heshima yao.

Mbowe alitoa kauli hiyo wakati akihutubia wananchi wa Kyela, mkoani Mbeya wakati akiwanadi wagombea wa nafasi mbalimbali kupitia chama hicho kwenye kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema kuwa pamoja na chama hicho kupitia katika mawimbi mengi, kimeendelea kusimamia na kuwa chama kikuu cha upinzani kwa sababu ni mpango wa Mungu kuwapo.

"Chama chetu ni imara, kimepigwa mawimbi mengi, lakini kwa kuwa ni mpango wa Mungu hakiwezi kufa kwa sababu ya visa. Kipindi cha miaka saba, kuna wengine hatukufa 'mazee...' lakini cha mtema kuni tulikipata. Sasa tumevuka bonde la uvuli wa umauti, tusiendelee kulalamika, tujipange kwenda mbele na hakuna kukata tamaa, kesho yetu iliyo bora zaidi inakuja.

"Tunapokwenda kwenye uchaguzi huu, tunaanza tena kurejesha heshima ya CHADEMA iliyoporwa kwa kukamata vitongoji, vijiji na mitaa, kikaongoze misingi huku chini," alisema.

Mbowe alisema chama chao kimejengwa kwa gharama kubwa, ikiwamo kwa kupitia dhoruba mbalimbali ambazo hata hivyo hawakukata tamaa kukipigania.

Mbowe alisisitiza kuwa hata kama chama hicho kikishika madaraka, licha ya kupitia vipindi vigumu vya ujenzi wa demokrasia, hakitakuwa tayari kuwa na visasi.

"Ujenzi wa demokrasia ya nchi hii kwa zaidi ya miaka 30, unataka kuchagua viongozi wanaoaminiwa na watu, CHADEMA siku tutakapokamata madaraka, hatutafanya kisasi, kisasi ni kazi ya Mungu, tutasimamia haki kwa sababu kwa taifa lisilo na haki haliwezi kuwa na baraka za Mungu," alisema Mbowe.

Alisema chama hicho kimejengwa kwa misingi mikuu minne; haki, uhuru wa watu, kuamini katika demokrasia na maendeleo ya watu, hivyo kitaendelea kuisimamia kikishika madaraka.

"Ukisema wewe ni mwana-CHADEMA, usiangalie sura ya Mbowe, tafakari misingi hiyo inayounda chama hiki, tangu kimeasisiwa, kimepambana na mawimbi yote kwa sababu kina imani na si maigizo, ninaomba imani hii ndiyo iwaimarishe," alisema.

**ACT WAZALENDO**

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akiwanadi wagombea wa chama chake katika kijiji cha Kajima, kata ya Kajika, jimboni Tunduru, alisema safari hii wamejipanga kudhibiti alichokiita "uporaji" katika uchaguzi huo.

"Sisi tumevumilia sana kuibiwa, mwaka 2020 tuliibiwa, na safari hii wamejaribu kutubipu tumewapigia, pengine huko walipo wanajipanga eti wajaribu kutuibia tena, ninawaambia simu zetu tumeweka bando la kifurushi cha mwaka, ataumia mtu safari hii, sisi tumejiandaa, tumejipanga, tusikubali haki yetu ya kuongoza kijiji iporwe," alisema Ado.

**TAMKO LA RAIS**

Kupitia tamko lake la Novemba 22 mwaka huu lililotangazwa rasmi jana, Rais Samia ametangaza tarehe 27, 2024 kuwa siku ya mapumziko kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, tamko hilo limetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Sikukuu za Kitaifa, Sura 35, kinachompa Rais mamlaka ya kutangaza siku yoyote kuwa ya mapumziko kama nyongeza ya siku zilizoainishwa kwenye jedwali la sheria hiyo au kubadili siku yoyote kati ya zilizoainishwa na siku hiyo kuwa ya mapumziko kama vile imetajwa kwenye jedwali la sheria.

"Na kwa kuwa tarehe 27 Novemba 2024, Jumatano, ambayo ni siku ya kazi, imetangazwa na waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa kuwa siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024, Rais anakusudia kutangaza Siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwa siku ya mapumziko," inasomeka sehemu ya tangazo hilo lililotolewa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI jana.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya na Romana Mallya**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Bil.200/- kutatua mabadiliko tabianchi Tanga

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MABADILIKO ya tabianchi yanayoukabili Mkoa wa Tanga kutokana na mafuriko, mvua zisizotabirika na ongezeko la joto, yameanza kutafutiwa ufumbuzi, kupitia mradi wa Green & Smart Cities Programme (SASA).

Mradi huo unaofadhiliwa na Umoja wa mabalozi wa nchi za Ulaya, kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), utatumia zaidi ya Sh. bilioni 200 kutekeleza mradi huo.

Kwa mujibu wa Meneja Programu wa GIZ, Dk. Fredy Lerise, mradi huo pamoja na mambo mengine unakusudia kujengea uwezo taasisi na mtu mmoja mmoja katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

"Suala hili ni kubwa kwa nchi zetu hasa kwa upande wa mafuriko, mvua zisizotabirika pamoja na ongezeko la joto ambalo kwa Jiji la Tanga limeonekana kuwa ni tatizo kubwa linaloongezeka," alisema.

Aidha, alisema GIZ inafanya kazi na Wizara ya Maji na mamlaka zake, ambapo wamesaidia upatikanaji wa huduma kidijitali kwa kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa vizuri.

"Tunafanya kazi na mamlaka za maji za mikoa ya Mwanza na Tanga, lakini pia wasimamizi wa rasilimali za maji kwa Bonde la Mto Pangani, ili kuwapatia uwezo wa kupanga mipango ambayo utapunguza ukosefu ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa maendeleo endelevu," alisema.

> **"Kutakuwa na ujenzi wa masoko mawili lakini pia wanawake na vijana watajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo mbalimbali ili waweze kupiga hatua za haraka kimaendeleo.**

Baada ya ujio wa mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa mitatu ya Mwanza na Tanga kwa Bara na Pemba kwa Zanzibar.

Alisema Jiji la Tanga limenufaika huku lengo kubwa ni ubia kati ya wafadhili, serikali kuu pamoja na serikali ya jiji hilo ambao ndiyo watekelezaji.

"Kutakuwa na ujenzi wa masoko mawili lakini pia wanawake na vijana watajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo mbalimbali ili waweze kupiga hatua za haraka kimaendeleo.

"Lakini pia kutakuwa na uwezeshaji wa kiuchumi, kwahiyo ni mradi muhimu sana na utatekelezwa kwa muda wa miaka minne na baada ya hapo tunategemea tutaendelea nao na kufikia malengo tuliyokusudia," alisema.

Alitoa wito kwa wanufaika wa mradi huo kuweka mbele maslahi ya jamii na kupata matokeo endelvu kwa kujifunza na kutumia mafunzo hayo kwa umma badala ya kutanguliza maslahi yao binafsi.

Hata hivyo, aliwaasa wasimamizi wa miradi hiyo kufanya kazi zao kwa weledi na uaminifu kwa kuleta matokeo mazuri kwenye miradi bila kufanya ubadhirifu kwa lengo la kujinufaisha wenyewe.



Msimamizi wa Mradi wa Shirika la Kilimo endelevu Tanzania (SAT), Yohana Malecela (kulia), akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Kandasikira wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, kuhusu mbinu za kilimo ikolojia, usimamizi bora wa malisho na lishe ya mama na mtoto, mafunzo yaliyonufaisha zaidi ya watu 10,000 wa vijiji 10 jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Madiwani wafura kusuasua ujenzi wa kiwanda

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUSUASUA kuanza kwa mradi mkubwa wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata parachichi katika Wilaya ya Hai, Kilimanjaro, 'kumeliamsha' Baraza la Madiwani la Wilaya la Hai kumwazimia mwekezaji aliyesaini mkataba wa ujenzi huo.

Ujenzi wa kiwanda hicho, unalenga kuongeza fursa za kiuchumi kwa wakulima wa parachichi, ambao kwa sasa wamekuwa wakitegemea wanunuzi binafsi, huku baadhi wakilalamikia bei ya kuyumba.

Akizungumza jana katika kikao cha baraza la madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji, Dionis Myinga, Ofisa Ushirika na mwanasheria kwenda kumkumbusha mwekezaji juu ya mkataba wake na kumsukuma kuanza utekelezaji. Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alipopewa nafasi ya kutoa ushauri wake alisema: "Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kiti chako kielekeze sasa, yule ambaye amesaini mkataba wa kisheria kujenga kiwanda cha parachichi, kupitia azimio hili asukumwe ili aanze kujenga, kwa sababu wananchi wengi wamepokea mwamko wa kupanda zao hilo.

"Inakuwaje wanakuja watu wanachukua parachichi wanapeleka Kenya, lakini kwa bei chee. Huyu mtu tungemsimamia akatekeleza mkataba wake wa kisheria ambao ulisainiwa mchana kweupe.

...Sasa hivi tunatafuta namna mbadala ya kuweza kufanya kuimarisha na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja, ndiyo maana tukaja na uwekezaji kwenye zao la parachichi."

Chama cha Ushirika cha MROSOSANGU, kilitia mkataba na mwekezaji huyo na kusimamiwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Nchini.

"Kwenye mkataba ule kwenye Chama cha MROSOSANGU, ambako tumempata mwekezaji James (mzungu), tulikubaliana kabla ya mwaka 2025 awe ameanza kujenga kiwanda cha parachichi. Kiwanda ambacho kitachukua parachichi za kisasa na ile reject kwa ajili ya kutengeneza mafuta," alisema.

Kwa mujibu wa Saashisha ametembelea na kukagua eneo hilo lakini mpaka sasa mwekezaji hajaanza kazi hiyo.

Akisoma maazimio ya baraza hilo, Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, Zephania Gunda, alisema azimio la kwanza linawahusu wakulima ambao wanamiliki maeneo ya kilimo.

Azimio la pili, ni kwa wakulima wenye uwezo washauriwe kujenga viwanda vya kusindika parachichi, kwa kuwa tayari baadhi ya wakulima wanazalisha parachichi katika halmashauri.

Tayari, China imefungua soko jipya la parachichi zinazozalishwa nchini baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutia sahihi mkataba wa mauzo ya zao hilo na serikali ya nchi hiyo.

Soko hilo litaongeza kiwango cha parachichi kinachouzwa nje ya nchi kwa sasa kutoka tani 12,000 hadi tani 10,000.

# Mabeyo akoshwa ujenzi nyumba wanaohama Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** HANDENI

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Jenerali Mstaafu, Venance Mabeyo, ameridhishwa na mradi wa nyumba 2,500 za wananchi waliohama kwa hiari katika hifadhi hiyo na kwenda katika Kijiji cha Msomera, Handeni, mkoani Tanga.

Jenerali Mstaafu Mabeyo, alikagua mradi huo Msomera iliyoko Kata ya Misima na kujionea pia ujenzi wa miundombinu ya maji, mawasiliano, barabara, minada, majosho, kituo cha kuuzia maziwa, shule, zahanati, shule na maeneo ya malisho yaliyotengwa na serikali.

"Nazipongeza sekta zote zinazohusika kutekeleza mradi huu hapa Kijiji cha Msomera, kwa kukamilisha nyumba 2,500 na miradi mingine muhimu.

"Tumetembelea eneo la Block F (Kitalu F), ambapo nyumba 1,000 zimekamilishwa katika awamu ya kwanza, iliyohusisha ujenzi wa nyumba 5,000.

...Kitalu hiki pekee kuna matangi matatu ya maji, yenye ujazo la lita 300,000 kwa kila moja. Tangi lingine la ujazo wa lita 650,000 linajengwa. Hii inathibitisha kuwa wananchi wanaopisha shughuli za uhifadhi Ngorongoro, wakija hapa watafurahia maisha yao."

Awali Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando, aliwahakikishia wananchi wa Ngorongoro wanaohamia eneo hilo kuwa hali ya usalama ni shwari.

Aidha, Kaimu Kamanda wa operesheni ya ujenzi wa nyumba za Msomera, Kitwai na Saunyi, Luteni Kanali, Edward Mwanga, alimweleza Jenerali Mstaafu Mabeyo na bodi yake kuwa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT), wamekamilisha ujenzi wa nyumba zote 2,500 kwa asilimia 100.

Luteni Kanali Mwanga, alisema nyumba hizo ni za kisasa na ubora wa hali ya juu, hivyo kwa sasa wanahamishia nguvu kwenye ujenzi wa nyumba nyingine 2,500.

Alisema kati ya hizo, nyumba 1,000 zitajengwa Kijiji cha Saunyi, Wilaya ya Kilindi (Tanga) na nyumba 1,500 zitajengwa Kijiji cha Kitwai B, Wilaya ya Simanjiro (Manyara).

Mwakilishi wa Kamishna wa Uhifadhi NCAA, Gloria Bideberi, alisema uongozi wa NCAA, utahakikisha kuwa kazi ya uelimishaji na uhamasishaji kwa wananchi inaendelea kwa kasi zaidi ili wananchi waliopo Ngorongoro waendelee kuhamia Msomera.





# Vyama vya siasa, polisi wakutana kujadili amani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

VYAMA vya siasa mkoani Mwanza, wadau wa uchaguzi pamoja na Jeshi la Polisi wamekutana kujadili namna ya kushirikiana kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unakuwa wa amani na haki na kuzuia matumizi ya nguvu.

Mkutano huo uliongozwa juzi na Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Wilibroad Mutafungwa na kuvieleza vyama pamoja na wadau hao kuwa mpaka sasa hali ya amani na utulivu vimeimarika zaidi, hivyo kuwataka kuilinda wakati wote wa uchaguzi.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kutojihusisha na mikusanyiko isiyokuwa halali ambapo wakiwa kinyume na agizo hilo Jeshi la Polisi litalazimika kuutawanya mkusanyiko huo, litalazimika kuchukua hatua kali na kuwa viongozi wa vyama wanapaswa kusimamia ratiba walizopewa ili kuimarisha amani.

**"Hatutahitaji vikundi vyovyote vitakavyoleta uvunjifu wa amani, hivyo watu wasije wakajichanganya wakawa na magenge hayo, tumejipanga ...**

"Hatutahitaji vikundi vyovyote vitakavyoleta uvunjifu wa amani, hivyo watu wasije wakajichanganya wakawa na magenge hayo, tumejipanga vizuri kuwadhibiti watakaoonyesha viashiria vya kuvunja amani na hatutamwonea huruma mtu yoyote," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kadhalika, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura na kurejea nyumbani.

Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Mwanza, Boniphace Nkobe, alisema hakuna mtu atakayefanya uvunjifu wa amani na kuwa uchaguzi utafanyika katika hali ya amani.

Aidha, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, Mkoa wa Mwanza (MNEC), Jamali Babu, alilitaka Jeshi la Polisi kutimiza wajibu wake na kutoa fursa kwa wadau wa uchaguzi kutambua wajibu wao katika uchaguzi huo.

Alisema watawaelekeza wanachama wao kuhakikisha wanafuata sheria, taratibu na kanuni ili baada ya uchaguzi maisha mengine yaendelee.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Zanzibar, Salumu Mwalimu, akiwanadi wagombea wa chama hicho, ili wapate ridhaa ya kuwaongoza wananchi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, pembeni yake ni wagombea wa nafasi za mwenyekiti wa mtaa, kijiji, kitongozi na wajumbe kwenye mkutano uliofanyika Kata ya Kagongwa, Manispaa ya Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ukosefu wa maji chanzo mabinti kupata mimba Kishapu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

HALI ya mabadiliko tabianchi na ukosefu wa huduma ya majisafi katika Kijiji cha Kiloleli wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, kumetajwa kuwa sababu ya kukithiri kwa matukio ya mabinti kupata mimba za utotoni.

Hayo yalibainishwa juzi na mabinti kijijini hapo wakati wakizungumza na Nipashe ilipotembelea, kuona namna athari za mabadiliko ya tabianchi zinavyosababisha madhara kwa vijana na watoto kupitia sekta ya maji.

Mmoja wa mabinti hao, Victoria Mlimandago, alisema wanapokuwa wakifuata maji nyakati za usiku katika kijiji jirani cha Ukenyenge, wanarubuniwa na wavulana na baadhi yao hukubali na hatimaye kupata ujauzito.

"Hapa kijijini tunakabiliwa na shida kubwa ya majisafi na salama, tunaiomba serikali ituletee maji ya Ziwa Victoria, sisi mabinti tunapata shida ya kurubuniwa kufanya mapenzi na wavulana tunapofuata maji usiku, mwisho wa siku tunaambulia mimba za utotoni," alisema Victoria.

Baadhi ya vijana akiwamo, Nkuba Jilala, alikiri baadhi yao hufanya mapenzi na mabinti wanapofuata maji nyakati hizo za usiku, huku wakilalamikia pia ukosefu wa maji kijijini hapo ambao kumewaathiri kwa kupoteza muda wa kufanya shughuli za kimaendeleo.

Mkazi mwingine katika kijiji hicho, Kwangu Madaha, alisema ukosefu wa majisafi na salama kijijini hapo licha ya kuchochea mimba za utotoni pia umekuwa ukisababisha migogoro ya ndoa pindi wanapochelewa kurudi nyumbani.

"Hapa maji hufuatwa kijiji jirani cha Ukenyenge umbali wa kilomita 17, wanafuata mara nyingi vijana kwa mikokoteni ya ng'ombe na hukohuko hupeana ujauzito," alisema Kwangu. Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kishapu, Diksoni Kamazima, alikiri kijiji hicho kutokuwa na huduma ya majisafi na salama na kubainisha kwamba mpango upo wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria ili kumaliza tatizo hilo.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024/25 kuna mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria utatekelezwa ukiwa na thamani ya Sh.bilioni 5.9, ambao utatoka Kata ya Mwamashele kupitia Lagana, Ngofila hadi Kiloleli.

Alisema mwaka jana serikali kupitia mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi ili jenga bwawa la maji katika kijiji hicho cha Kiloleli, lengo likiwa ni kuwaondolea adha wananchi ya ukosefu wa maji.

Alisema lakini wananchi hao walieleza kuwa maji hayo hayafai kwa matumizi ya binadamu, bali kunyweshea mifugo.

# 'Mtakaochaguliwa uchaguzi S/mitaa msilete ubaguzi'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAASISI ya Maendeleo kwa Viziwi Tanzania (TAMAVITA) imewataka viongozi watakaopata ridhaa ya kuchaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwajali watu wenye ulemavu katika kuwapatia huduma bora bila ubaguzi.

Pia wametakiwa kuhakikisha majengo mapya ya umma yanayojengwa yanakuwa na miundombinu rafiki dhidi yao.

Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Kelvin Nyemba alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu namna watu wenye ulemavu watakavyoshiriki katika uchaguzi huo.

Alisema baadhi ya viongpzi wa serikali za mitaa waliopita walikuwa wakiwabagua watu wenye ulemavu katika kuwapatia huduma, hasa wanapofika katika ofisi zao na wengi walipoteza haki zao walizokuwa wakizipigania hasa za umiliki wa viwanja.

"Katika uchaguzi huu sisi pia tunahaki ya kuchaguliwa kama yalivyo makundi mengine, ulemavu tulionao usitumike kutunyanyapaa majukwani kuwa hatuna uwezo wa kuongoza wananchi na pia viongozi watakaopata nafasi ya kuchaguliwa wahakikishe wanatuhudumia vema bila ya ubaguzi wowote," alisema Nyemba.

Alisema asilimia mbili za mikopo zinazotolewa na halmashauri mchakato wake unaanzia ngazi za serikali za mitaa, hivyo wawapitishie nyaraka zao bila ya kuwaomba fedha.

Aidha, aliziomba kamati za ulinzi na usalama kwa kushirikiana na TAMISEMI kuweka utaratibu mzuri ili watu wenye ulemavu waweze kushiriki vema katika uchaguzi huo, kwamba endapo ikitokea fujo au vurugu siku ya uchaguzi watakaopata madhara ni wao.

Hivyo, alisihi kundi hilo kujitokeza tarehe tajwa na kuchagua viongozi bora na wanaowahitaji.

Mgombe wa CHADEMA katika Mtaa wa Kagongwa Manispaa ya Kahama, James Mshima, alisema kujali watu wenye ulemavu ni moja ya kipaumbele chake.

Alisema endapo akipata ridhaa atahakikisha anawasimamia na kupata mkopo wa asilimia mbili ili waweze kujikimu kimaisha kupitia biashara.

Mgombea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mtaa wa Nyahanga, Benard Mapalala alisema tangu awali alikuwa akihakikisha wenye ulemavu wanapata haki sawa na makundi mengine.

Hivyo, aliwataka viongozi wao kushirikiana pamoja katika kuibua miradi mipya ambayo itawaingizia kipato na kuondokana na utegemezi.

Nipashe
# Spotika



KOCHA MPYA WA MANCHESTER UNITED, RUBEN AMORIM UK. 13




# RASHFORD, GARNACHO MTIHANI KWA AMORIM

**MANCHESTER,** England

KUNA aina mbili za maumivu ya kichwa wakati ukiwa kocha wa mpira wa miguu; moja, majeraha yanamaanisha huna wachezaji wa kutosha na ni changamoto kuchagua timu; mbili, kwa sababu una chaguzi nyingi na lazima ufikirie mchanganyiko bora wa wachezaji wako.

Hali hiyo sasa inajidhihirisha kwa Kocha Mkuu mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, pale linapokuja suala la safu ya ushambuliaji.

Mreno huyo anatumia mfumo wa 3-4-3 ambao ulimpa matokeo mazuri akiwa Sporting CP.

**United bado ina matatizo katika safu ya beki wa kati, huku Harry Maguire akiwa nje ya uwanja, Lisandro Martinez akijiondoa kwenye kikosi cha Argentina na Victor Lindelof akiwa ameumia alipokuwa na kikosi cha Sweden.**

Marcus Rashford, Alejandro Garnacho na Amad Diallo kila mmoja ana uwezo wake binafsi, na pia wanaweza kucheza kila upande. Lakini wote wana jukumu linalopendelewa na Amorim atahitaji kufikiria jinsi ya kuwatumia ili kupata matokeo bora zaidi kutoka kwa watatu hao.

**Marcus Rashford**

Mfungaji bora zaidi katika kikosi cha Manchester United kilichopo ni Rashford. Ingawa hajacheza vizuri kwa takriban miezi 18, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alifunga mabao 30 wakati wa msimu wa 2022/23. Pia alikuwa amevuka mabao 20 katika misimu miwili kati ya mitatu kabla ya hapo. Namba za aina hizo hazifanyiki kwa bahati mbaya, hivyo kwa mara nyingine tena, anatakiwa kutoa kwa Amorim.

Rashford amecheza zaidi kutoka upande wa kushoto katika miaka ya hivi karibuni, ingawa mechi kadhaa msimu huu amekuwa upande wa kulia. Anajua pia kucheza katikati.

Wakati alipoingia kwenye timu mwaka 2016, alicheza zaidi kati, lakini kwa Amorim ni wazi kwamba Rashford atafaa zaidi upande wa kushoto.

**Alejandro Garnacho**

Hapa ndipo matatizo yanapoanzia, kwa sababu Alejandro Garnacho pia kimsingi ni winga wa kushoto. Huko ndiko alikofunga mabao sita kati ya saba msimu huu. Kwa hiyo ikiwa Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 20, atacheza katika timu moja na Rashford, mmoja wao hatakuwa katika nafasi anayoipenda zaidi uwanjani, jambo ambalo limekuwa hivyo mara kadhaa katika miezi ya hivi karibuni.

Hivi sasa, Garnacho ana ufanano mkubwa na Cristiano Ronaldo wakati akiwa katika umri huo. Ni wazi jinsi alivyo na kipaji, na tayari ana uwezo wa kujiondoa katika matukio madhubuti ya kubadilisha mchezo. Ambacho Garnacho anahitaji kuimarika uthabiti.

**Amad Diallo**

Kati ya hao watatu, Amad Diallo ndiye anayestarehe zaidi upande wa kulia, lakini pia ndiye aliyepata nafasi kidogo zaidi.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast, alisajiliwa kwa mkataba wenye thamani ya euro milioni 37 alipokuwa kijana asiyejulikana mwenye umri wa miaka 18.

Tayari huu ni msimu wake wanne akiwa na United na amecheza kwa mkopo kule Rangers na Sunderland.

Amad alianza msimu huu vizuri, lakini akakosa nafasi kisha akakosa nafasi wakati wa utawala wa Erik ten Hag, kabla ya kupata nafasi tena wakati wa muda wa Ruud van Nistelrooy.

Kama Amorim anataka winga wa asili wa kulia, mwenye umri wa miaka 22, Amad ndiye anayefaa zaidi.

## ISIKUPITE

KIPIGO cha mabao 4-0 ilichokipata Manchester City dhidi ya Tottenham juzi kinawakilisha msururu mrefu zaidi wa kupoteza katika maisha ya ukocha kwa Pep Guardiola, na mbaya zaidi tangu 2006 chini ya Stuart Pearce. Lakini pia hii ni mara ya kwanza kwa City kupoteza mechi tatu mfululizo za Premier League chini ya Guardiola, pia hakuwahi kupoteza mchezo wowote wa ligi nyumbani kwa mabao manne katika maisha yake ya ukocha.



# WASHAMBULIAJI 6 WANAOWEZA KUMRITHI LEWANDOWSKI BARCA

**BARCELONA,** Hispania

ROBERT Lewandowski amekiri kwamba, hajioni akicheza zaidi ya misimu miwili au mitatu ijayo, akifichua kwamba anataka kustaafu kwa wakati unaofaa.

Kwa sasa, mshambuliaji huyo mkongwe wa Poland bado anapachika mabao akiwa na Barcelona na anaongoza katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu.

Lakini pia itakuwa ni makosa kwa wababe hao wa Katalunya kutokuwa tayari kuzingatia kitakachofuata.

Barca hawajaondoka kwenye hali mbaya ya kifedha, lakini bado wameonesha katika miaka ya hivi karibuni uwezo wa kutoa mikataba mikubwa.

Wachezaji kama Dani Olmo (ana mkataba wa euro milioni 60, Raphinha (euro mil. 58), Jules Kounde (euro mil. 50 na hata Lewandowski (euro mil. 45).

Makala haya yanaangazia washambuliaji sita ambao Barcelona wanaoweza kuwazingatia kama mbadala wa Lewandowski, twende sasa...

**Viktor Gyokeres**

Msimu uliopita ulikuwa wa kwanza kwa Viktor Gyokeres katika mashindano ya juu, akiwa hajawahi kucheza mchezo wa Ligi Kuu England kwa misimu minne akiwa na Brighton & Hove Albion.

Lakini alifunga mabao 21 kwenye michuano ya EFL na 29 kwenye Ligi Kuu ya Ureno na tangu hapo hajaangalia nyuma.

Raia huyo wa Sweden ambaye sasa ana umri wa miaka 26, tayari ana mabao 23 kwa jina lake katika mashindano yote msimu huu. Ubaya ni bei, na Sporting wanaweza kutaka hadi euro milioni 100 kwa mchezaji huyo.

Hata hivyo, Barcelona watakabiliwa na upinzani kutoka timu kama Manchester United, Arsenal na Chelsea.

**Omar Marmoush**

Omar Marmoush hivi karibuni alifikia rekodi ya Lionel Messi katika ligi tano bora za Ulaya kwa kufunga mkwaju wa faulo wa moja kwa moja katika mechi tatu mfululizo, ambapo gwiji huyo wa Camp Nou alifanya hivyo miaka mitano iliyopita.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri, amekuwa akijenga jina lake akiwa na Eintracht Frankfurt kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akianza maisha baada ya kujiunga na klabu hiyo mwaka 2023 kwa uhamisho wa bure baada ya kipindi kigumu katika klabu ya awali ya Wolfsburg.

Frankfurt wanaelewa kuwa kumuuza Marmoush hakuwezi kuepukika, lakini watataka euro milioni 40 kumwachia. Hapo awali walimuuza Randal Kolo Muani kwa euro milioni 90 mwaka 2023.

**Jonathan David**

Mshambuliaji mmoja bora ambaye atapatikana bila ada ya uhamisho mwishoni mwa msimu ni Jonathan David. Lille tayari wamekubali kumpoteza raia huyo wa Canada kama mchezaji huru, baada ya kushindwa kukubaliana kuhusu mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amezifumania nyavu mfululizo katika maisha yake yote ya soka hadi sasa kwenye soka la Ubelgiji na Ufaransa, hajawahi kufunga chini ya mabao 12 ya ligi katika misimu yake yote sita kamili, na ana wastani wa mabao 17 katika kila kampeni.

Katika kila moja ya misimu miwili iliyopita, amefunga mabao 26 katika mashindano yote na tayari yuko mbioni kuvuka idadi hiyo, kwani kwa sasa ana mabao 13.

**Marcus Thuram**

Kuna uhusiano wa kifamilia hapa kwani baba yake, Marcus Thuram, Lilian, akitumia misimu miwili ya mwisho ya maisha yake ya soka pale Camp Nou kati ya mwaka 2006 na 2008.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa sasa ni nyota anayetambulika kivyake, akifurahia msimu mzuri wa kwanza na Inter Milan wa 2023-24 na amekuwa tena na mwanzo mzuri wa msimu wa 2024/25, akiwa na mabao saba katika mechi 12 za Serie A hadi sasa.

Thuram aliripotiwa kulengwa na Liverpool chini ya kocha Jurgen Klopp na sasa inasemekana kuwa yupo kwenye rada za viongozi hao wa Ligi Kuu England wakiwa na kocha Arne Slot.

Kifungu cha kuruhusiwa kuondoka cha euro milioni 85 kinaweza kikawa kikwazo kikubwa kwa Barcelona.

**Samu Aghehowa**

Samu Aghehowa hakika amefanya vema msimu huu. Mshambuliaji huyo mwenye jeraha hivi karibuni aliitesa Manchester United wakati Porto ilipomenyana na Waingereza hao kwenye Ligi ya Europa, baada ya kuhama kutoka Atletico Madrid wakati wa majira ya kiangazi kwa kitita cha euro milioni 15.

Hiyo ilikuwa baada ya dili la Chelsea ambalo thamani yake ni karibu mara tatu zaidi kushindikana, lakini haijamzuia Samu kuimarika katika msimu wake wa pili katika soka la wakubwa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amecheza katika kikosi cha Luis de la Fuente cha Hispania.

Aghehowa ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 100, ambacho bado kinaweza kuchukuliwa kuwa thamani nzuri kutokana na umri wake na uwezo wake.

Hata hivyo, Atletico Madrid wana haki ya kupata asilimia 50 kwa mauzo yake.

**Mohamed Salah**

Ingawa si mbadala wa moja kwa moja wa Lewandowski katika suala la nafasi uwanjani, Mohamed Salah bila shaka anaweza kuchukua nafasi ya kufunga mabao.

Kiukweli wawili hao wanaweza kuishia kucheza pamoja kutokana na dirisha la upatikanaji wa Salah kuwa msimu ujao wa majira ya joto ikiwa hatasaini mkataba mpya na Liverpool na Lewandowski hatarajiwi kuondoka Barcelona hivi karibuni.

Hata hivyo, Salah si suluhu la muda mrefu pia, lakini Lewandowski alikuwa karibu kutimiza umri wa miaka 34 aliposajiliwa kutoka Bayern Munich na haukuwa mpango mbaya kabisa kwa Barca.

Nyota huyo wa Misri kinadharia anaweza kuchukua jukumu la Lewandowski na kulibeba kwa miaka michache mbele.

Kocha wa Liverpool Slot tayari amependekeza kuwa atacheza hadi mwisho wa miaka thelathini kama vile Lionel Messi au Cristiano Ronaldo.



THURAM

## Nukuu

"Naweza kuwa mwenye tabasamu, lakini tunapokuwa na kazi ya kufanya nitakuwa mtu tofauti, kuna sehemu za kufurahia, lakini naweza kuwa mkatili inapobidi. [Naweza] kuwa mtu mzuri zaidi ambaye utawahi kuona, lakini ikiwa kuna mtu anayejifikiria tu, nitakuwa mtu tofauti," **Kocha mpya wa Manchester United, Ruben Amorim.**



"Katika miaka minane hatukuwahi kuishi hivi. Nilijua mapema au baadaye tungeshuka. Sikutarajia kupoteza mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu, lakini tumekuwa na msimamo wa ajabu tena na tena na tena. Sasa hatuwezi kukataa ukweli kwamba wakati mwingine hutokea kwenye soka na maisha yapo hapa," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola baada ya kipigo cha mabao 4-0 juzi nyumbani dhidi ya Tottenham.**



"Nimemwona Ethan Nwaneri mara kadhaa na yeye ni maalum zaidi. Arsenal iliwaacha Kai Havertz na Declan Rice nje na hata hatukugundua," **Winga wa zamani wa Scotland, Pat Nevin, aliiambia BBC Radio 5 Live baada ya kinda huyo wa miaka 17 kuifungia Arsenal juzi ikishinda 3-0 dhidi ya Nottingham Forest.**



# HIVI NDIVYO STARS ILIVYOFUZU AFCON MARA ZOTE NNE



Winga wa Taifa Stars, Simon Msuva, akisababisha hatari kwenye lango la Guinea katika mchezo wa Kundi H, kusaka tiketi ya kucheza fainali za AFCON zitakazochezwa mwakani nchini Morocco. Katika mchezo huo uliochezwa, Novemba 19, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Stars ilishinda bao 1-0 na kufuzu fainali hizo.

**Na Adam Fungamwango**

NOVEMBA 19, mwaka huu, ikiwa ni mwezi mmoja tu kabla ya miaka 63 ya Uhuru, timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, ilifanikiwa kutinga fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa mara ya nne.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 60 lililowekwa wavuni na winga wa Kimataifa, Simon Msuva, anayecheza soka la kulipwa katika Klabu ya Al Talaba ya Iraq.

Ikiwa kwenye Kundi H, Stars ililazimika kuifunga Guinea ili kumaliza nafasi ya pili nyuma ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Hii ni mara ya nne kwa Tanzania kuweza kufuzu fainali hizo tangu ilipojipatia uhuru wake kutoka kwa Waingereza, Desemba 9, 1961.

Kombe la Mataifa ya Afrika ndiyo michuano mama ya kimataifa katika Bara la Afrika, inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Ilianza kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 1957. Kuanzia mwaka 1968 ilianza kuchezwa mara moja kila baada ya miaka miwili.

Mataifa matatu ndiyo yaliyoanza kucheza michuano hiyo ambayo ni Misri, Sudan na Ethiopia, huku Afrika Kusini ambao walikuwa nao wanataka kushiriki, walizuiwa kutokana na sera za ubaguzi wa rangi wakati huo. Baada ya hapo ikaitwa michuano ya Mataifa Huru barani Afrika, ili kuzuia nchi za Afrika ambazo hazijawa huru na zinazotawaliwa kimabavu, zisitie mguu.

Kwa maana hiyo zikawa zinashiriki timu za Afrika zilizopata uhuru, na zilicheza kwa mtindo wa mtoano na baadaye kupata timu nane ambazo zilikuwa zinacheza fainali zake kwa kuzigawa makundi mawili, A na B.

Fainali hizo zikaitwa Fainali za Mataifa Huru barani Afrika. Na mfumo huo uliochezwa baada ya nchi kadhaa kupata uhuru na kuongeza idadi ya timu.

Kwa sasa nchi zote za Afrika zimepata uhuru na mfumo wa kupata washindi wanaoingia kwenye fainali hizo umebadilika, ikijulikana sasa kama michuano ya AFCON.

Katika makala haya, tunaiangazia safari ya Tanzania ilipokuwa ikitinga fainali hizo kwa mara zote nne.

**1. Tanzania 2-1 Zambia (1979)**

Stars ilianzia raundi ya kwanza dhidi ya Mauritius, ambapo katika mchezo wa kwanza ugenini Mauritius, Aprili 16, 1979, ilichapwa mabao 3-2, kabla ya kupindua meza nyumbani kwa kuinyuka nchi hiyo mabao 4-0 nchini, Aprili 29, 1979.

Ilikuwa Agosti 11, 1979 jijini Dar es Salaam, Stars iliposhinda bao 1-0 dhidi ya Zambia kwenye mchezo wa raundi ya pili lililowekwa wavuni na Mohamed Rishard 'Adolf', huku mchezo wa marudiano, Ndola Zambia, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Alex Chola aliwapatia wenyeji bao dakika ya 43, kisha Peter Tino kusawazisha dakika sita kabla ya mechi kumalizika.

Matokeo ya jumla ya mabao 2-1, yaliifanya Stars kufuzu fainali hizo ambazo zilichezwa 1980, nchini Nigeria.

Kwenye fainali hizo, Stars ilishika nafasi ya mwisho kwa kucheza mechi tatu, ilipoteza mbili na sare moja, ikiwa Kundi A pamoja na timu za Ivory Coast, Misri na wenyeji Nigeria wakifuzu. Nigeria ndiyo waliokuwa mabingwa mwaka huo baada ya kuifunga Algeria mabao 3-0 katika mchezo wa fainali.

**2# Tanzania 3-0 Uganda (2019)**

Tanzania ilifuzu kwa mara ya pili 2019 ilipoifunga Uganda, The Cranes mabao 3-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Machi 24.

Ilikuwa ni miaka 40, baada ya kufuzu mara ya kwanza 1979 nchini Zambia, fainali zake zikichezwa 1980 nchini Nigeria.

Yalikuwa ni mabao ya Msuva dakika ya 21, Erasto Nyoni kwa mkwaju wa penalti, dakika ya 51 na Aggrey Morris.

Matokeo hayo yaliifanya Stars kumaliza nafasi ya pili kwa pointi nane, nyuma ya Uganda iliyokuwa na pointi 13 kwenye Kundi L.

Fainali zake zilichezwa Julai nchini Misri, Stars ikiwa Kundi C, ilimaliza ikishika mkia, safari hii haikupata pointi yoyote, ikipoteza mechi zote tatu dhidi ya Kenya, Senegal na Algeria, bingwa kwa mara nyingine akitoka kwenye kundi lake, nayo ni Algeria, iliyoifunga Senegal bao 1-0.

**3# Tanzania 0-0 Algeria (2023)**

Tanzania ilifuzu kwa mara ya tatu AFCON 2023, ambapo fainali zake zilichezwa nchini Ivory Coast.

Ikiwa Kundi F na timu za Uganda, Niger na Algeria, ilifanikiwa kumaliza nafasi ya pili nyuma ya Algeria iliyokuwa na pointi 16, yenyewe ikimaliza na pointi nane.

Stars ilihitaji sare tu dhidi ya Algeria na ilifanikiwa kuipata ugenini, Septemba 7, 2023 na kufikisha pointi nane, ikiiacha Uganda na pointi zake saba.

Fainali zake zilichezwa kuanzia Januari 13, mwaka huu, hadi Februari 11, Tanzania ikiwa Kundi F na timu za Morocco, DR Congo na Zambia, kwa mara ya tatu ilishika mkia, lakini safari hii ilipata pointi mbili, ikipoteza moja na sare mbili.

**4# Tanzania 1-0 Guinea (2024)**

Kwa mara nyingine imepata tena tiketi ya kucheza AFCON mara ya nne. Msuva kwa mara ya pili amehusika kufunga bao la kuipeleka Stars fainali kama ilivyokuwa 2019. Stras haijawahi kushinda mechi yoyote ya fainali za AFCON mara zote tatu ilizocheza. Je, mwakani nchini Morocco kwenye fainali hizo Tanzania itatoka kimasomaso?

## JE, WAJUA?



ETHAN Nwaneri mzaliwa wa London (umri wa miaka 17 na siku 247) amekuwa mchezaji wa pili kwa umri mdogo kufunga bao kwenye Ligi Kuu England kwa Arsenal, nyuma ya Sesc Fabregas pekee (miaka 17 na siku 113 mnamo 2004), ambaye baada ya hapo alishinda Kombe la Dunia akiwa na Hispania. Nwaneri alifunga bao hilo juzi wakati Arsenal ikishinda 3-0 dhidi ya Nottingham Forest.



## Tanzania, Norway, SAGCOT kuendeleza sekta ya kilimo

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA na Norway pamoja na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) zimeingia makubaliano ya miaka mitatu ya kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba huo, Balozi wa Norway nchini, Tone Tinnes matokeo ya ushirikiano huo ni undugu uliojengwa baina ya mataifa hayo kwa miaka 14.

Alisema mkataba huo utakaoanza mwaka 2025 hadi 2027 unalingana na vipaumbele vya Norway katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, usalama wa chakula na kilimo endelevu.

Alisema mkataba huo ni matokeo ya ziara aliyofanya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini Norway Februari 2024.

"Ushirikiano huu unajengwa juu ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan na kusainiwa kwa makubaliano ya maelewano ya kuimarisha ushirikiano wa kilimo na miaka 60 ya ushirikiano kati ya nchi zetu," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya SAGCOT, Dk. Ally Laay, alisema: "Mkataba huu ni hatua nyingine muhimu katika kutekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan za kuendeleza na kuinua sekta ya kilimo."

Alisema mkataba huo utawezesha SAGCOT kuimarisha miradi yake ya msingi, ikilenga uvumbuzi, uendelevu, na ukuaji wa uchumi katika sekta ya kilimo.

Dk. Laay alisisitiza kuwa fedha zilizotengwa zitatumika kimkakati kwa mujibu wa mpango wa kimkakati wa SAGCOT wa 2025-2027 ili kufanikisha athari zinazopimika.

Alibainisha kuwa ushirikiano kati ya SAGCOT na Norway umebadilisha sekta ya kilimo Tanzania kwa kiasi kikubwa, kwamba zaidi ya hekta 859,298 zimesaidia wakulima wapatao 900,000.

Alisema pia mapato ya wakulima yameongezeka hadi Dola za Marekani milioni 254, huku uwekezaji ukifikia Dola za Marekani bilioni 1.3 kutoka sekta binafsi na Dola za Marekani bilioni 2.2 kutoka sekta ya umma.

Alisema mkataba huo unaimarisha maono ya pamoja kati ya Tanzania na Norway kuhusu kilimo endelevu, usalama wa chakula, na ukuaji wa uchumi shirikishi.

# Wasafirishaji kemikali wapewa angalizo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, amezitaka kampuni binafsi zinazotumia na kusafirisha kemikali kutoa elimu kwa umma na wafanyakazi wao ili kulinda afya na mazingira.

Alitoa wito huo juzi wakati akizungumza katika hafla ya kuhitimisha kampeni ya utoaji elimu kwa umma juu ya usafirishaji salama wa kemikali hatarishi ya Sodium Sianidi. Kamanda Katabazi alisema kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Namba 3 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2020 zilitungwa kwa lengo la kulinda afya na mazingira.

Alibainisha kuwa katika utekelezaji wake, sheria na kanuni zimeweka masharti mbalimbali ili kuwezesha kemikali hizo kuendelea kuingia nchini, kuhifadhiwa, kusafirishwa na kutumiwa bila kuleta madhara kwa afya na mazingira.

**Alisema kuwa matumizi na faida za kemikali ni nyingi na hazina mbadala katika maisha ya kila siku ya binadamu kwa kuwa zimekuwa zikitumika katika sekta...**

Alisema moja wapo ya masharti ya msingi katika utekelezaji wa sheria hiyo ni utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya wafanyakazi mahala pa kazi na jamii ambayo inakuwa kwenye hali hatarishi ya kemikali hizo.

"Pamoja na sharti hili la kutoa elimu linapaswa kutekelezwa na serikali pamoja na sekta binafsi. Lakini ni kampuni chache ndiyo zinatoa elimu kwa wafanyakazi wao na jamii inayowazunguka juu ya madhara ya kemikali na jinsi ya kuepuka yasitokee. Nazipongeza kampuni chache zinazotekeleza na kutimiza takwa hili kisheria kwa maana hatujawahi kupata kesi kuwa kuna madhara yametokea," alisema.

Alisema kuwa matumizi na faida za kemikali ni nyingi na hazina mbadala katika maisha ya kila siku ya binadamu kwa kuwa zimekuwa zikitumika katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, kilimo, viwanda, maji na madini.

Hata hivyo alisema kemikali hizo zisipotumika kwa kufuata na kuzingatia taratibu zilizowekwa ndani yake zimebeba hali hatarishi kwa afya na mazingira.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali nchini kutoka Ofisi ya Mkemia, Daniel Ndiyo, alisema kemikali ni sumu na ina uwezo wa kuwaka moto wenye sumu hivyo ni lazima jamii na wasafirishaji wajengewe uelewa ili kulinda afya na mazingira.

Msimamizi Mkuu wa Usafirishaji kutoka Kampuni ya Barrick, Joseph Mbanya alisema elimu imetolewa kwa makundi mbalimbali ikiwamo Jeshi la Polisi, wadau wa afya na anaami-




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwa na viongozi wengine wakishuhudia Meneja wa Mradi Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Japhet Senyinah, akitia saini na mkandarasi wa kampuni ya Otonde Construction and General Supplies Limited, Amos Milanzi, mkataba wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Masimba utakaogharimu Sh. bilioni 10.496. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

# Bilioni 10/- zatengwa ujenzi skimu ya umwagiliaji vijiji 5

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAKAZI 24,000 wa vijiji vitano katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida watanufaika na kilimo cha umwagiliaji baada ya serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NiRC) kutoa Sh. bilioni 10.496 kwa ajili ya ujenzi mradi wa skimu ya Masimba.

Mkurugenzi Idara ya Uendelezaji Miundombinu, Raphael Laizer, akizungumza juzi wakati wa hafla ya kukabidhi mkandarasi kuanza kazi ya ujenzi wa mradi huo, alisema wakazi watakaonufaika ni kutoka vijiji vya Masimba Urugu, Mlandala Mang'ole na Ujungu.

Laizer ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa, katika hafla hiyo, alisema kazi zitakazofanyika ni pamoja na ukarabati wa bwawa na sehemu ya utoro wa maji, kuchimba mchanga na tope ndani ya bwawa ili kuongeza ujazo wa bwawa kufikia mita za ujazo 250,000.

Alisema kazi nyingine zitakazofanyika ni ujenzi wa mfereji mkuu kwa kiwango cha zege na ujenzi wa mfereji wa mita 9,254 kwa kiwango cha zege.

Naye Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema serikali inatekeleza miradi mingi ya kilimo cha umwagilia nchini, lengo ni kuboresha maisha ya Watanzania kupitia sekta ya kilimo.

Alisema mradi huo utakapokamilika utawawezesha wananchi kulima mara tatu na kwamba kinachofanywa na serikali ni kutaka kuwaondolea wananchi umaskini kupitia sekta ya kilimo.

Aidha, aliipongeza Wizara ya Kilimo kwa jinsi inavyoitendea haki sekta ya kilimo akisema hakuna miujiza katika uchumi zaidi ya mapinduzi yanayofanywa na sekta hiyo inayogusa watu wengi kupitia umwagiliaji.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema ni faraja kuanza utekelezaji wa mradi huo kwani kilikuwa kilio cha muda mrefu kwa wakulima wa eneo hilo.

Mwenda alisema wilaya yake ina chakula cha kutosha kwani mwaka jana zilizalishwa tani 308,000 za chakula wakati mahitaji ni tani 90,000.



# Mbowe awaita wana-CHADEMA kushiriki uchaguzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewataka wananchi mkoani Mbeya kuhakikisha wanashiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha wanawachagua viongozi wenye sifa.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipokuwa anazungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara wa uzinduzi wa kampeni za uchaguzi ambapo alisema Ofisi ya Serikali ya Mtaa ndiyo Ikulu ya wananchi wa eneo husika.

Hivyo, aliwataka wananchi kuwachagua viongozi wanaotokana na chama hicho akidai kuwa ndiyo wenye uwezo wa kutatua kero zao, huku akisisitiza kuwa Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa mitano ambayo chama hicho kimesimamisha wagombea wengi.

Alisema endapo wananchi watawachagua wagombea wa CHADEMA itakuwa ndiyo mwanzo mzuri wa kurejesha madiwani wengi, wabunge na hata kupata rais anayetokana na chama hicho kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani.

Alisema chama hicho kitahakikisha kinarejesha majiji yote ambayo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 yalikuwa yanashikiliwa na chama hicho hasa wabunge na madiwani.

**Alisema chama hicho kitahakikisha kinarejesha majiji yote ambayo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 yalikuwa yanashikiliwa na chama hicho hasa wabunge na madiwani.**

Alisema katka Uchaguzi Mkuu wa mwaka mwaka 2015 ndiyo uchaguzi ambao ulikuwa wa mafanikio zaidi kwa chama hicho kutokana na kuongoza majiji yote nchini pamoja na kupata zaidi ya wabunge 80.

Alisema uchaguzi huo ndiyo ulikuwa wa mwisho kuwa wa kidemokrasia na kwamba baada ya hapo haujawahi kufanyika tena uchaguzi wa kidemokrasia.

Alisema kutokana na vyama vya upinzani kukandamizwa katika kipindi cha miaka saba, baadhi ya vyama hivyo vimepoteza nguvu isipokuwa viwili ambavyo ni CHADEMA na ACT Wazalendo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi 'Sugu', alisema kwenye maeneo mengi nchini wananchi hawapati maendeleo kwa sababu wanaongozwa na wenyeviti wa serikali za mitaa ambao hawakuwachagua.

Alisema baadhi ya viongozi hao wamekuwa wakikwamisha maendeleo kwa kutafuna fedha ambazo zilitakiwa kutumika kujenga miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Huu ndio wakati sahihi wa kuwaondoa wenyeviti hao, chagueni wagombea wetu ambao tuna uhakika tumewaandaa vizuri, zimefanyika mbinu za kuwaondoa lakini hazijazaa matunda," alisema.

Pia aliwataka wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kuhakikisha wanawatendea haki wagombea wote ili kuepuka malalamiko ambayo yamekuwa yakiibuka kwenye kila uchaguzi.



Watumishi wa Wizara ya Afya wakisimamia shughuli ya uchangiaji damu iliyofanywa na madereva wa malori na mabasi ya mikoani kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wagombea CCM Lunyanywi 'wamwaga' sera zao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MGOMBEA wa nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Lunyanywi Kata ya Mjimwema katika Halmashauri ya Mji wa Njombe (CCM), Julius Lupenza, amesema endapo atachaguliwa atasimamia maboresho kwenye barabara za mtaa huo pamoja na kituo cha afya.

Lupenza alitaja vipaumbele hivyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa eneo la Hagafilo, Lunyanywi na Mjimwema ambapo aliwaomba wananchi wa eneo hilo kumuamini ili akatekeleze vipaumbele hivyo.

Alisema amejipanga vizuri kuhakikisha anahudumia wananchi kwa kusikiliza kero zao na kuzitatua kwa wakati bila ya kuwasababishia adha wala vikwazo.

"Nafahamu mtaa wetu hatuna ofisi tunatumia majengo ya shule lakini pia barabara zetu za mitaa zinahitaji maboresho makubwa pamoja na kituo chetu cha afya mkinichagua nitahakikisha namshirikisha diwani na mbunge wetu ili changamoto hizi ziishe," alisema Lupenza.

Nao wagombea nafasi ya wajumbe wa Mtaa wa Lunyanywi akiwamo Sabasi Ndauka alisema kuteuliwa kwao kukiwakilisha CCM haikuwa kwa bahati mbaya hivyo ameahidi kwenda kutumikia wananchi kwa haki na wajibu.

Mgombea nafasi ya Mwenyekiti Mtaa wa Mjimwema, Nuhu Masasi, alisema anasababu ya msingi ya kugombea nafasi hiyo kwa sababu ya kutaka kuyaendeleza mambo yote ya maendeleo yaliyofanywa na CCM.

Baadhi ya wananchi Kata ya Mji Mwema, akiwamo Lucas Sanga alisema viongozi hao licha ya kuomba kura pia wajipange kwa dhati kuhudumia wananchi.

Jane Mbilinyi alisema wamejipanga vizuri kushiriki uchaguzi huo na kutoa rai kwa viongozi kutotumia nafasi hiyo kujinufaisha.

Uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika nchini kote Novemba 27, mwaka huu.

# Polisi yawahakikishia usalama waandishi wa habari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUELEKEA Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, Jeshi la Polisi mkoani Mbeya limewahakikishia usalama waandishi wa habari wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Pia, limetoa mafunzo maalumu kwa waandishi kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao bila kupata madhara wakati wa kampeni za uchaguzi, wakati wa kupiga kura na wakati wowote zinapotokea vurugu hasa za kisiasa.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alisema waandishi wa habari ni kundi muhimu na hivyo linapaswa kulindwa.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuhakikisha makundi yote yanayoshiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanakuwa salama na kwamba kutokana na hali hiyo ndiyo maana liliamua kuanza kutoa mafunzo ya kwa wadau hao.

Alisema kabla ya kutoa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari walishatoa kwa viongozi wa vyama vya siasa ili na wao washiriki katika kuhakikisha uchaguzi huo unamalizika kwa amani na utulivu bila kutokea kwa mushkeli wowote.

"Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, alituita ma-RPC wote nchini kwa lengo la kuweka mikakati ya kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu, na sisi tumeona ni vema tuyatoe kwa wadau ambao tunafanya nao kazi. Kwa hiyo waandishi ni miongoni mwa wadau muhimu, msiwe na wasiwasi," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwasisitiza waandishi wa habari kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao ili kuepuka kuingia kwenye migogoro ambayo itawafanya wasitekeleze vizuri majukumu yao.

Alisema jeshi hilo lipo imara na litahakikisha linasimamia sheria, kanuni na taratibu wakati wa uchaguzi na kwamba halitasita kuchukua hatua kwa yeyote atakayebainika kukiuka taratibu hizo.

Hata hivyo Kamanda Kuzaga aliwataka waandishi wa habari kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanatumia taaluma zao kuandika mambo ambayo yataisaidia jamii ikiwamo kuelezea mchakato wa uchaguzi unavyofanyika.

Baadhi ya waandishi wa habari walilalamika kuhusu uwepo wa matukio ya waandishi kukamatwa na polisi wakati wa kutekeleza majukumu yao licha ya kuwa na vitambulisho hali ambayo inawapa hofu wanapofanya shughuli zao.

Mmoja wa waandishi hao, Anthony Komba alisema wakati wa kutekeleza majukumu yao waandishi wanakuwa na vitambulisho vyao vya kazi, lakini inapotokea Jeshi la Polisi linawakamata watu wanaodhaniwa kuwa wahalifu na waandishi wanaunganishwa.

Mkuu wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Charles Kinyongo alisema jeshi hilo limeimarisha ulinzi na usalama wakati wote ili kuhakikisha shughuli zote zinafanyika kwa amani na utulivu.



# Serikali yaeleza mikakati kuboresha huduma ya umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaibu Hassan Kaduara, amesema serikali inalenga kutafuta vyanzo vya ndani vya uzalishaji wa nishati ya umeme pamoja na kuweka miundombinu imara ya kusafirishia, ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya huduma hiyo.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa kujadili maendeleo ya nishati, hotuba yake ikisomwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi.

Alisema Zanzibar ina ongezeko kubwa la miradi ya uwekezaji hasa katika sekta ya utalii hali inayosababisha kuongezeka kwa mahitaji ya nishati ya hiyo.

Alisema kuwa miradi hiyo ni kivutio kwa uchumi wa Zanzibar lakini haiwezi kufikiwa iwapo nishati ya umeme haitakuwa ya uhakika.

"Sasa hivi tunahitaji kufanya uchunguzi kuhusu umeme wa upepo na umeme wa bahari, sasa mkutano huu umeshirikisha wadau ambao wana utaalamu zaidi, hivyo watatuongoza katika kuyafikia malengo hayo," alisema Kilangi.

Aidha, alisema kuwa, serikali kupitia ZESTA inafanya maboresho ya mfumo wa umeme kupitia mkopo nafuu wa Benki ya Dunia (WB) ambapo vituo viwili vya kupozea umeme Makunduchi na Matemwe vinatarajiwa kujengwa ili kusaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo hayo.

Alisema kuwa serikali imeweka mikakati zaidi katika kuhakikisha kuwa nishati ya umeme inapatikana na kuondoa changamoto hasa kushirikiana na wadau wake wa maendeleo.

Akizungumzia kuhusu matumizi ya nishati mbadala ya kupikia alisema mkutano huo utajadili kuhusu nishati safi ya kupikia ili kupunguza uharibifu wa mazingira pamoja na kuwakinga wananchi na madhara ya kiafya yanayotokana na matumizi ya nishati inayotokana na kuni na mkaa.

Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Haji Haji, alisema shirika hilo limejipanga kuleta maboresho makubwa ya mfumo wa umeme ili kupunguza changamoto ya kukatika kwa umeme.

Alisema shirika hilo linaendelea kupunguza gharama za uungaji umeme pamoja na kuondoa msongamano wa maombi ya kuunganishwa na huduma hiyo ili kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Mwakilishi kutoka Benki ya Dunia, Rhanda Jordan alisema kuwa malengo ya mkutano huo ni kujadili changamoto katika sekta ya nishati na umeme.

Alisema kuwa serikali kupitia wizara hiyo imekuwa na malengo ya kuhakikisha kuwa nishati ya umeme inapatikana kwa uhakika.

# Wajasiriamali 112,000 wasajiliwa programu ya Samia

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAJASIRIAMALI 112,500 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wamesajiliwa katika Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA).

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng' Issa, aliyasema hayo katika mkutano wa imarisha uchumi na Mama Samia kwa wajasiriamali wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema kuwa katika programu hiyo wanasajili watu katika mfumo, kwamba hadi sasa wameshasajili wajasiriamali 112,500 Bara na Visiwani. Alisema kuwa wanaamini takwimu hizo zitaongezeka na kupata idadi kubwa zaidi.

Beng' alisema kuwa jambo ambalo wameliona kwenye mizunguko yao katika mikoa hiyo, kupitia programu hiyo kwanza ni mwitikio wa watu kuwa mkubwa.

Alisema kuwa Mkoa wa Kusini Pemba walifanikiwa kupata watu 1,300 na hata Kaskazini watu waliweza kujitokeza kwa wingi.

Alisema wapo wenye uwelewa lakini wengi wao ambao hawana uwelewa ni jinsi gani anaweza kupata hiyo mikopo na ni vigezo gani anatakiwa kuwa navyo, ili aweze kufanikisha bila changamoto yoyote.

**Alisema kuwa jambo lingine ambalo wameliona ni kuwapo kwa wafanyabiashara kufanya biashara zao zisizokuwa rasmi...**

Aidha, alisema kutokana na changamoto hiyo matukio yake mtu anaweza kukata tamaa na kuona kama vile serikali haimsaidii.

Alisema kuna haja watu kupewa taarifa juu ya programu za kuongeza ujuzi lazima ziwepo na kuwafanyia mafunzo ili kupata zile taarifa na kupata uhalisia wa jambo linalotakiwa.

Alisema kuwa jambo lingine ambalo wameliona ni kuwapo kwa wafanyabiashara kufanya biashara zao zisizokuwa rasmi, biashara ambazo hazijasajiliwa na kutokuwa na akaunti za benki, jambo ambalo linapelekea kutotambuliwa na mamlaka ya mapato.

Alisema kuwa kitu kingine walichokiona ni fursa za manunuzi ya umma, serikali imepitisha sera ya kusaidia wafanyabiashara wadogo na wakati kufanya biashara na serikali kupitia zabuni.

Alisema watahakikisha kila mkoa wanapata vipaumbele kupitia IMASA, kwenye miradi mbalimbali ikiwamo kilimo cha mboga na uvuvi, kwani kila mkoa unakuwa na kipaumbele chake.

Hivyo, aliomba suala hilo lifanyiwe kazi kwa kutolewa mafunzo na kupata vigezo vinavyotakiwa ili kuingia kwenye kupata hizo fursa.


Mshauri wa Rais katika masuala ya wanawake na makundi maalum, Sophia Mjema alisema kuwa IMASA ipo kwa ajili ya kuwaondoa wananchi katika hali ya umaskini na kuwaweka kwenye uchumi wa kati.

Alisema kuwa IMASA lengo lake kubwa ni kuhakikisha wananchi wanainuka kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kuziamini serikali zao, ili waendeleze kuwapatia maendeleo mengine zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema kuwa programu hiyo itakuwa chachu ya maendeleo kwa wananchi nchini.

Alisema kuwa mfumo huo haukulenga kwenye kundi moja bali umelenga katika makundi mbalimbali kama ambavyo umekusudiwa kufanya kazi zake kwa maendeleo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiandika jina lake, wakati alipozindua mradi wa mauzo wa nyumba za Chumbuni zinazojengwa na Shirika la Nyumba Zanzibar katika ukumbi wa mikutano Hoteli ya Amani, Mkoa wa Mjini Magharibi. **PICHA IKULU**

# Wasaidizi wa sheria wapunguza migogoro katika jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, amesema wasaidizi wa sheria wamesaidia kuondoa migogoro ya wananchi katika maeneo yao.

Alisema hayo juzi wakati akifungua Jukwaa la Nne la Msaada wa Sheria Zanzibar na kusema kuwa wananchi wengi Zanzibar wanamwamko wa kujua mambo ya kisheria.

Alisema kujua masuala ya kisheria na imekuwa dawa ya kuondokana na migogoro katika jamii zao na kabla ya hapo kulikuwa na changamoto nyingi zikiwakabili na kusababisha migongano kwa jamii.

Alisema kuwa wasaidizi wa msaada wa kisheria wanawigo mkubwa wa kuwafuata wananchi, kuwapa elimu juu ya kutambua haki zao.

Alisema kuwa wadau wa maendeleo wanawajibu wa kuendelea kuwasaidia wasaidizi hao na wamekuwa watu muhimu kwa jamii ya chini hasa kwa watu wasio jiweza.

Alisema kuwa kauli mbiu ya mwaka huu isemayo 'Ushawishi wa upatikanaji wa rasilimali za kuendeleza huduma za msaada wa kisheria Zanzibar' inaonesha wa wazi kuwa jambo hilo lina umuhimu wake katika jamii.

Waziri huyo alisema kuwa jukwaa hilo lina umuhimu wake na litakuwa dira ya kujadili mambo mbalimbali na changamoto juu ya kufanya kazi kwa watu hao kwa maendeleo ya jamii hasa wa vijijini.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mansura Mossi Kassim, alisema kuwa wasaidizi wa msaada wa kisheria wana wajibu wa kutoa elimu ndani ya jamii ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa mambo ya sheria.

Mwakilishi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Ali Shaibu alisema wamefarijika kuona namna wasaidizi wa msaada wa kisheria Zanzibar wanavyofanya kazi zao kwa ubunifu.

Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhan Said, alisema malengo ya kuwapo kwa wasaidizi wa msaada wa kisheria limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na elimu inayotolewa na wasaidizi hao ndani ya jamii.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Katiba na Sheria Tanzania, Edith Shekidele, alisema wataendelea kushirikiana na idara ya katiba na msaada wa kisheria Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 27275 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GORDON KILABO MENGO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY SEKELA SAMSON MWAKIBWILI……………..PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 10 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19 Day of 12, 2024
Dated at Dodoma this 19 Day of 11, 2024.
Dated at Dodoma this 19 Day of 11, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 29095 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ADELAIDE COSMAS CHENGELELA DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

**CHRYSANTUS ALPHONCE MIZAMBWA…………..1st PETITIONER**
**HERIETH CHRYSANTUS MIZAMBWA……………..2nd PETITIONER**
**…………………………………………………………3rd PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 12 day of DECEMBER.2024
Dated at MOROGORO this 19TH day of NOVEMBER.2024

PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO DISTRICT COURT

---

## KADI ZA GARI ZIMEPOTEA

Ndugu **RAJABU ISSA NGUMBI** anatangaza kupotelewa kwa kadi za gari zenye usajili ufuatao; **T.177 ADZ aina ya SUZUKI ESCUDO, T.759 BVE** aina ya **LAND CRUISER, T.860 CTU** aina ya **CARINA.** Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/709/2024**

---

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

Ndugu **RAJABU ISSA NGUMBI** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili.**T.943 CAW aina ya SANLG**. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu nawe. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/709/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.97/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AMINA MUSSA BAMBALI wa MAILIMBILI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SULTANI ABDALLAH HASSAN**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU

---

**KIBAIGWA AUCTION MART**
**P.O.BOX 20,**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KIBAIGWA AUCTION MART, KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA GARI MOJA AINA YA SUBARU LEGACY YENYE NAMBA ZA USAJILI T 875 DDE MALI YA NYANGE JOHN KIBOKO , BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 20/12/2024 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NDUGU FRANSISCO ALBERT KINYAIYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC 142EEC. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba: **PHQ/GEI/GEI/10284/2024**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DUCUMENTS ACT**
**(CAP 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEPOLL**

THIS CHANGE OF NAME DEED is made this 31st the day of OCTOBER 2024 by me RESTO PAULO YUSUPH, formerly known FESTO P YUSUPH, FESTO PAULO MROPE and FESTO PAULO YUSUPH of Nachingwea District within Lindi Region, now or until recently called me FESTO PAULO YUSUPH, FESTO P YUSUPH and FESTO PAULO MROPE.
That the name of FESTO PAULO MROPE it appear in my National Identity Card with reference number 20000412653040000124
That the name of FESTO P YUSUPH is registered at my National Voter's Card with reference number T328502709149
That the name of FESTO PAULO YUSUPH it appear in my Certificate of Secondary Education

**WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED as follows:-**

- I absolutely renounce and abandon the use of my said former names of FESTO PAULO MROPE and FESTO P YUSUPH and I assume and determine to take and use the new name of FESTO PAULO YUSUPH in substitution of my former names of FESTO PAULO MROPE and FESTO P YUSUPH AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I DECLARE I shall at all the time hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and in occasions whatsoever use the new name of FESTO PAULO YUSUPH in substitution of my former name of FESTO PULO MROPE and FESTO P YUSUPH so relinquished as aforesaid to the indent that I may hereafter be known not by the aforesaid former name, but by the new name of FESTO PAULO YUSUPH only.
- AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE all personat all times to describe and address me by the new name of FESTO PAULO YUSUPH.

IN WITNESS whereof I have hereinto subscribed my new of FESTO PAULO YUSUPH and have affixed my signature the day and year name written.



---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**RODRICK FIDELIS MATUNDA** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria yenye namba TAE152482 ambayo imetolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mnamo tarehe 30/07/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/45118/2024.**

---


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA




Wajumbe wakipiga makofi katika mkutano wa mwisho wa kikao kwenye Kongamano la Umoja wa Mataifa la Mabadiliko ya Tabianchi la COP29, mjini Baku, Azerbaijan jana. **PICHA: REUTERS**

## MABADILIKO TABIANCHI...

# Trilioni 795/- kutolewa kwa nchi maskini

**Na Maulid Mmbaga**

ULIMWENGU umekubaliana na mkataba mpya wa hali ya hewa huku nchi tajiri zikiahidi kutoa dola bilioni 300 (Sh. trilioni 795) kila mwaka ifikapo 2035 kwa nchi maskini ili kuzisaidia kukabiliana na athari zinazoongezeka za janga la hali ya hewa.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana katika mkutano wa COP29 uliokuwa ukifanyika huko Baku, Azerbaijan, huku nchi nyingi zinazoendelea zikikosoa kiwango cha fedha hizo kwamba hazitoshi.

Makubaliano hayo yanakuja baada ya zaidi ya wiki mbili za migawanyiko mikali na mazungumzo yaliyovurugika, yaliyotupwa katika machafuko na kususia, kurushiana maneno ya kisiasa na sherehe za wazi za nishati ya mafuta.

Rais wa COP29, Mukhtar Babayev, anaeleza kuwa kulikuwa na wasiwasi kwamba huenda makubaliano hayo yamesusiwa na mataifa yenye uchumi duni lakini hadi kufikia tamati ya mazungumzo yao nchi zaidi ya 200 zilikubaliana na adhimio hilo.

Anaeleza kuwa Sh. trilioni 795 zitaenda kwa mataifa yaliyo hatarini, maskini zaidi ili kuwasaidia kukabiliana na hali mbaya ya hewa inayozidi kubadilisha uchumi wao kuelekea nishati safi.

"Imekuwa safari ngumu, lakini tumewasilisha mpango," anasema Simon Stiell, Mkuu wa Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi.

"Lengo hili jipya la kifedha ni sera ya bima kwa ubinadamu, huku kukiwa na athari mbaya ya hali ya hewa inayoikumba kila nchi," amesema Stiell.

Inaelezwa kuwa kiasi kilichoahidiwa, kinapungua kwa kiasi cha dola trilioni 1.3 za wanauchumi waonasema zinahitajika kusaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na mzozo wa hali ya hewa licha ya kwamba kumekuwa na majibu ya hasira kutoka kwa nchi nyingi zinazoendelea.

Katika hotuba ya mwakilishi wa India Chandni Raina alikashifu dola bilioni 300 kama kiasi kidogo, na kuyaita makubaliano hayo kwamba si chochote zaidi ya udanganyifu wa macho na hayawezi kushughulikia ukubwa wa athari zinazojitokeza.

Mjumbe wa hali ya hewa wa Visiwa vya Marshall Tina Stege, anasema wameondoka na sehemu ndogo ya ufadhili wa nchi zilizoathiriwa na hali ya hewa, huku akikosoa vikali mazungumzo hayo kama yanaonyesha fursa mbaya zaidi ya kisiasa.

"Masilahi ya mafuta yamedhamiriwa kuzuia maendeleo na kudhoofisha malengo ya kimataifa ambayo tumefanya kazi kuyajenga," amesema Stege.

**MKATABA ULIVYO**

Inaelezwa kuwa COP29 ililenga sana fedha, suala muhimu la hali ya hewa lakini mojawapo ya mikataba iliwasilishwa zaidi kisiasa.

Nchi tajiri, ambazo zinawajibika kwa kiasi kikubwa kwa mabadiliko ya hali ya hewa ya kihistoria, zilikubali mwaka 2009 kutoa dola bilioni 100 kwa mwaka ifikapo 2020 kwa nchi zinazoendelea.

Ahadi hiyo, ambayo tayari inatazamwa kuwa haitoshi, ilifikiwa tu mnamo 2022, miaka miwili iliyopita wakati wa mwisho.

Pia mkataba huo mpya uliokubaliwa Jumamosi unazitaka nchi tajiri, zikiwamo Marekani na mataifa ya Ulaya, kutoa dola bilioni 300 kila mwaka ifikapo 2035, zinazojumuisha fedha za umma na binafsi.

Ingawa makubaliano hayo pia yanarejelea azma pana ya kufikia dola trilioni 1.3, mataifa yanayoendelea yalitaka nchi tajiri kujitolea kuchukua sehemu kubwa zaidi ya hiyo na pesa kuja kwa kiasi kikubwa katika mfumo wa ruzuku badala ya mikopo. Na kwamba wanahofia watawatia mtegoni zaidi katika madeni.

Inaelezwa kuwa kundi la G77 la nchi zinazoendelea lilikuwa limetaka kiasi cha dola bilioni 500, lakini mataifa tajiri yalikataa takwimu za juu zaidi kama zisizo za kweli kutokana na hali ya sasa ya kiuchumi.

"Tumefika kwenye mpaka kati ya kile kinachoweza kufikiwa kisiasa leo katika nchi zilizoendelea na kile ambacho kingeweza kuleta mabadiliko katika nchi zinazoendelea," amesema Avinash Persaud, mshauri maalum wa mabadiliko ya hali ya hewa kwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Amerika ya Kati.

Kulikuwa pia na msukumo kwa mataifa tajiri yanayoibukia kiuchumi kama vile China na Saudi Arabia kuchangia katika mfuko wa ufadhili wa hali ya hewa, lakini makubaliano hayo yanahimiza tu nchi zinazoendelea kutoa michango ya hiari, na haitoi wajibu wowote kwao.

Li Shuo, Mkurugenzi wa Kituo cha Hali ya Hewa cha China katika Taasisi ya Sera ya Jumuiya ya Asia aliita makubaliano hayo kama maelewano yenye dosari ambayo yanaonyesha eneo gumu zaidi la kijiografia ambalo ulimwengu unajikuta.

Hata hivyo ilielezwa kuwa uharaka wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa haujawahi kuwa wazi zaidi, na kwamba huwenda awamu hii mkutano huo utatoa matokeo ya haraka.

**ANACHOSEMA TRUMP**

Katika hatua nyingine inaelezwa kuwa Rais Mteule wa Marekani, Donald Trump ameuita mzozo wa hali ya hewa kuwa ni uwongo, huku akiapa kuondoa taifa hilo kwenye makubaliano ya kihistoria ya hali ya hewa ya Paris, na kuzua wasiwasi juu ya mustakabali wa hatua za kimataifa.

Saudi Arabia, ambaye ni msafirishaji mkuu wa mafuta duniani, ambayo imesukuma dhidi ya hatua kabambe katika mikutano ya hali ya hewa iliyopita, ilionekana kuwa na ujasiri zaidi ikikataa hadharani na kwa uwazi marejeleo yoyote ya mafuta, makaa ya mawe na gesi katika makubaliano hayo.

Friederike Otto, mwanasayansi wa hali ya hewa katika Chuo cha Imperial London anasema "Imekuwa COP nyingine ya kivuli, iliyotiwa mafuta. Maslahi ya umma katika COP hii yamekuwa ya chini na wasiwasi unaweza kusababisha kuhisi kama umefikia kiwango cha juu."

**SINTOFAHAMU**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Hatua za Hali ya Hewa, Tasneem Essop, anasema yaliyojadiliwa katika mkutano huo yamekuwa mazungumzo ya hali ya hewa ya kutisha zaidi kwa miaka mingi kutokana na imani mbaya ya nchi zilizoendelea.

"Hii ilikusudiwa kuwa COP ya fedha, lakini 'Global North' ilikuja na mpango wa kusaliti 'Global South'," amesema Essop.

Anasema matokeo yanatoa matumaini ya uwongo kwa wale ambao tayari wamebeba mzigo mkubwa wa majanga ya hali ya hewa. Naye Harjeet Singh wa Mpango wa Mkataba wa Mafuta, anasema "Lazima tuendelee katika vita vyetu, tukidai ongezeko kubwa la ufadhili na kufanya nchi zilizoendelea kuwajibika."

**Chanzo Mitandao**

# FOUNTAIN GATE YAMWEKA SOKONI KINARA WA MABAO LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate, imemweka sokoni straika wake, Selemani Mwalimu, anayeongoza kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya 10, ikitaka kiasi cha Dola za Kimarekani 400,000 ili kumuuza.

Meneja Mwajiri wa Klabu hiyo, Muhibu Kanu, amesema kiasi hicho ambacho ni zaidi ya shilingi bilioni moja ya Kitanzania, ndiyo ada sahihi ya uhamisho ya mchezaji huyo kwa klabu yoyote inayomtaka.

"Kwenye mkataba wake Mwalimu kuna kipengele kinasema kuwa anaweza kununua mkataba wake kwa Dola 400,000 sawa na Sh. bilioni 1.06 za Kitanzania, klabu yoyote itakayotimiza hayo, tutafanya nao biashara hatuwezi kumzuia," alisema Kanu.

Kutokana na umahiri wake wa kupachika mipira ndani ya wavu, akiongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akipachika jumla ya mabao sita, tayari klabu kadhaa zimeshaanza kummezea mate straika huyo.

Straika huyo amefunga mabao matano kwa mguu wa kulia na moja kwa kutumia mguu wa kushoto.

Aliyofunga kwa mguu wa kulia, ni katika mechi dhidi ya Namungo, timu yake ikishinda mabao 2-0, Dodoma Jiji zikitoka sare ya 2-2, Kagera Sugar akiiongoza timu yake kushinda 3-1, dhidi ya Prisons, wakipoteza kwa 3-2 na KMC, Fountain Gate wakishinda 3-1.

Bao moja alilolifunga kwa mguu wa kushoto lilikuwa katika mchezo dhidi ya KenGold, timu yake ikishinda 2-1.

Mwalimu alisajiliwa na Fountain Gate akitokea KVZ ya Zanzibar, ambapo msimu uliopita alikuwa mfungaji bora wa ligi hiyo, akipachika mabao 20.



Mratibu wa pambano la ngumi la 'Fight for Change', Daniel Kijo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu pambano hilo linalotarajiwa kufanyika Dar es Salaam Jumamosi wiki hii. Wengine ni Bondia Karim Bhaloo na Hamis Mwintayi watakaopambana siku hiyo kwenye mchezo wa kick boxer. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Ngumi kutambulisha mchezo wa makofi Dar

**Na Faustine Feliciane**

PAMBANO la ngumi kuhamasisha vijana kuonesha vipaji vyao limepangwa kufanyika Jumamosi wiki hii jijini Dar es Salaam huku pia likitumika kutambulisha mchezo mpya wa kupigana makofi (Power Slash).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mratibu wa Pambano hilo, Daniel Kijo, alisema kutakuwa na mapambano ya mchezo wa kickboxer na ngumi za kawaida kwa mabondia wa Tanzania Bara na Zanzibar.

"Kutakuwa na mapambano 12, mabondia wote wamethibitisha kushiriki na kwa sasa wanaendelea na maandalizi ambapo tunategemea watapima uzito Novemba 29, mwaka huu," alisema Kijo.

Alisema lengo la mapambano hayo ni kuendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza michezo hususan ngumi na kuwapa nafasi vijana kuonesha uwezo na vipaji vyao.

Kwa upande wa mwanzilishi wa mapambano hayo ambaye ni bondia atakayepanda ulingoni siku hiyo, Karim Bhaloo, alisema wanatarajia pia kuutambulisha mchezo mpya wa kupigana makofi (Power Slash)

"Nimeanzisha hii shughuli kwa kutambua Tanzania kuna vipaji vingi sana, tutaleta nia kwa wale wenye uwezo wa kucheza ngumi na michezo mingine, lakini kubwa zaidi tutatambulisha mchezo mpya wa kupigana vibao, ni mchezo mgeni hapa kwetu, lakini nje ya nchi una umaarufu mkubwa," alisema Bhaloo.

Kwa upande wa mmoja wa mabondia wa mchezo wa ngumi na mateke (Kickboxer), Hamis Mwintayi, alisema amejiandaa vizuri kwa pambako lake dhidi ya Karim na kuwaomba Watanzania wawaunge mkono katika kuhamasisha mchezo huo.

Tiketi za pambano hilo litakalofanyika katika Ukumbi wa Pulse uliopo Masaki, Dar es Salaam tayari zimeshaanza kuuzwa.

# Wadau wataka wasanii wapewe elimu ya fedha

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa muziki nchini wamesema upo umuhimu wa wasanii wa fani hiyo nchini kupatiwa elimu ya uwekezaji ili iwasaidie kutumia vizuri vipato vyao vinavyotokana na kazi hiyo hasa pale shughuli zao hizo zinapofikia ukomo.

Walitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, katika hafla iliyowakutanisha wasanii hao kwa ajili ya kuwapatia elimu ya namna ya kutumia mifumo ya kidijitali kusambaza maudhui, iliyoandaliwa na Mdundo.Com.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya CRDB, Emmanuel Kiondo, alisema ipo mifano ya wasanii wengi ambao walifanikiwa kutengeneza fedha nyingi kupitia kazi hiyo lakini baadaye walirudi kuwa masikini baada ya kukumbwa na matatizo.

"Na hii yote inatokana na kukosekana kwa elimu ya fedha, kwamba msanii anakuwa na wakati mzuri, anafanya kazi na kutengeneza fedha, lakini badala ya kuwekeza, anatumia vibaya na mwisho wa siku anapopoteza uwezo wake wa kufanya shughuli yake hiyo anakufa masikini.

"Mtu badala ya kuwekeza fedha yake anayoipata kwa jasho, anaitumia vibaya katika mambo yasiyo ya msingi na akipata matatizo anapotea au wakati mwingine hata inabidi kuchangiwa. Kwa hiyo sisi kama CRDB, tunawapatia elimu ya namna ya kuwekeza kile wanachokipata, tunataka waache mambo ya kizamani," alisema Kiondo.

Mdau mwingine wa muziki, Aman Martin, alisema kuna haja ya kuongeza uelewa kwa wasanii wa muziki na wanaowasimamia ili wafahamu namna ya kutumia vizuri mifumo ya kidijitali katika kusambaza kazi zao.

Alisema bado kuna ugeni mwingi wa namna ya kutumia mifumo ya kidijitali katika kusambaza maudhui kwa wasanii wengi na kwamba kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wana kuwa na taarifa na maarifa ya kutosha ili iwasaidie kuepukana na shida ya kufanya kazi isiyo na manufaa.

"Tuachane na zile stori ambazo tumekuwa tukikutana nazo sana, kwamba mtu fulani alisaini mkataba ambao haukuwa na masilahi kwake, au mwingine hata hajui ni sehemu gani sahihi aiendee," alisema Martin.

Alisema bila kujali ni maarufu au laa, msanii akitumia vizuri mifumo ya kidijitali kusambaza maudhui ya kazi yake, ni rahisi kunufaika.

"Cha msingi ni wanamuziki hao kufahamu namna mifumo hiyo ya kidijitali inavyoendeshwa na namna ya kuitumia katika kuinua au kutangaza kazi zao," alisema Martin.

Maureen Njeri, Mkurugenzi Mkazi wa Mdundo.Com, alisema wao wamerahisisha kazi kwa kuwaunganisha wasanii wa muziki kutoa maudhui yanayofaa na kuyasambaza kwenda kwa jamii kwa lengo la kuhakikisha kila mmoja wao ananufaika na kazi hiyo.

"Na tunatoa kipaumbele kwa muziki wa nyumbani, hasa kwa nyimbo zinazoimbwa kwa lugha ya kiswahili, kwa hiyo tunatoa nafasi kwa wasanii kuitumia vema fursa hii," alisema Maureen.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AMORIM AMTAKA GYOKERES

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, ameweka kipaumbele cha kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres, kutoka klabu ya zamani ya Sporting msimu ujao, lakini Manchester City pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Sunday Mirror***)

### CAMAVINGA ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United imefanya mawasiliano na Real Madrid kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 22, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa hana nia ya kutaka kuondoka. (***Bernabeu Digital***)

### MENDES KWENYE RADA

MANCHESTER United pia inamfuatilia mlinzi wa pembeni wa Paris St-Germain, Nuno Mendes mwenye umri wa miaka 22, ambaye alicheza chini ya Amorim huko Sporting. (***Mail on Sunday***)

### ZIRKZEE SASA AGOMBEWA

ASTON Villa imejiunga na klabu kadhaa za Italia kuonesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23, kwa mkopo Januari. (***Caught Offside***)

### REIJNDERS ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inaweza kutoa ada kubwa kumnunua kiungo wa kati wa AC Milan na Uholanzi, Tijjani Reijnders mwenye umri wa miaka 26 msimu ujao. (***Fichajes***)

### WHARTON AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City inajitayarisha kumwania kiungo wa kati wa Crystal Palace, Adam Wharton, 20. (***Teamtalk***)

### HENRIQUE NA EVERTON

EVERTON inataka kumsajili winga wa Botafogo na Brazil, Luiz Henrique mwenye umri wa miaka 23, wakati huu kocha Sean Dyche akijaribu kuboresha safu yake ya ushambuliaji. (***Football Insider***)

### RENSCH AMULIKWA SPURS

KLABU za Tottenham Hotspur na Liverpool zimeungana na Barcelona katika mbio za kumsajili beki wa pembeni wa Uholanzi, Devyne Rensch mwenye umri wa miaka 21, kutoka Ajax. (***Diario Sport***)

### FERGUSON ANYATIWA


CHELSEA imebakia kuwa mashabiki wakubwa wa mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, lakini ‚Seagulls‘ hao watadai pauni milioni 100 kwa mchezaji huyo. (***TeamTalks***)

### DELAP NA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inaweza kukatiza mipango ya Chelsea ya kumsajili mshambuliaji wa Ipswich, Town Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, kwa kuwa wana kipengele cha kumnunua tena kwa pauni milioni 20 mchezaji huyo waliyemuuza msimu wa majira ya joto. (***Express***)

### MELLBERG HUYOOO MAREKANI

MLINZI wa zamani wa Sweden na Aston Villa, Olof Mellberg anatarajiwa kuchukua nafasi ya ukocha katika Klabu ya St Louis City inayoshiriki Ligi Kuu ya soka ya Marekani. (***Goal***)



# GUARDIOLA AKIRI MAJI YA SHINGO MAN CITY

## ●●● Sisi ni dhaifu kwa sasa, hiyo ni dhahiri, ikiwa hatushindi ni kwa sababu hatustahili...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kwamba kama Liverpool wataifunga Manchester City kwenye Uwanja wa Anfield wikendi ijayo, timu yake inaweza kuwa tayari imetoka kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

**City walipoteza mchezo wao wa tano mfululizo katika mashindano yote na mchezo wa tatu mfululizo wa ligi kwa kuchapwa mabao 4-0 na Tottenham Hotspur kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi.**

Kikosi cha Guardiola kitamenyana na Feyenoord kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho Jumanne kabla ya kusafiri hadi Anfield siku tano baadaye.

Liverpool jana Jumapili walikuwa na nafasi ya kusonga mbele zaidi kwa pointi nane kama walifunga Southampton na Guardiola aliulizwa baada ya kupoteza nyumbani dhidi ya Spurs ikiwa pengo la pointi 11 litakuwa ni sawa kwa City kupoteza matumaini ya ubingwa mbele ya kikosi cha Arne Slot, alijibu: „Ndio, ni kweli.“

“Hatufikirii kushinda au kupoteza taji, hatuko katika hali ya kufikiria juu ya kile kitakachotokea mwishoni mwa msimu.

“Ikiwa mwisho hatushindi ni kwa sababu hatustahili. Tulishinda huko nyuma kwa sababu tulistahili.

“Tunachopaswa kufanya sasa ni kuifunga Feyenoord. Hilo ndilo jambo muhimu zaidi - kwanza kwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya na hatua kwa hatua wachezaji watakuwa bora.“

Si tu kwamba City wamepoteza mechi tano mfululizo kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 18, pia wameruhusu mabao 14.

Majeruhi kwenye safu ya ulinzi wamekuwa wengi na kulikuwa na matatizo zaidi dhidi ya Spurs wakati John Stones alipolazimishwa kutolewa nje.

“Sisi ni dhaifu kwa sasa, hiyo ni dhahiri,“ alisema Guardiola.

“Lazima tuvunje matokeo kwa sababu ushindi unatusaidia kuwa chanya na kujiamini zaidi na lazima tufanye hivyo. Lakini baada ya miaka minane hapa nilijua mapema au baadaye tutashuka. Sikutarajia kupoteza mechi tatu za Ligi Kuu kwa mara moja lakini tumekuwa na msimamo wa ajabu tena na tena na sasa hatuwezi kukataa ukweli ambao wakati mwingine hutokea kwenye soka na maisha yapo hapa.“

HABARI MICHEZO

# ANCELOTTI: MBAPPE HAJAWAHI KUOMBA NAFASI REAL MADRID



**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amekanusha kuwa Kylian Mbappe anahitaji kucheza katika nafasi fulani au ameomba jukumu fulani uwanjani tangu ajiunge na kikosi hicho kipindi cha majira ya joto.

Kuwasili kwa Mbappe kwa uhamisho wa bila malipo baada ya kuondoka Paris Saint-Germain kulionekana kama mabadiliko mengine makubwa kwa timu ya Madrid ambayo ilikuwa imeshinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, Mfaransa huyo licha ya kufunga mara nane katika michuano yote, ameshindwa kuonesha ubora wake.

Madrid wamebadili mfumo tangu msimu uliopita wa ligi ya ndani na Ulaya ili kumweka Mbappe katika timu moja na Vinicius Junior na Jude Bellingham.

"Kylian hajawahi kuniomba nafasi uwanjani," alisema Ancelotti akiwambia waandishi wa habari.

"Wote wanataka kuwa kwenye kikosi cha kwanza, hawana nafasi maalum na wanaweza kubadilishwa kulingana na hali ya mechi.

"Washambuliaji wote wamekuwa na mwenendo sawa, wasipofunga wanachanganyikiwa.

"Ninamuona akiwa na ari na furaha kufanya mazoezi na wachezaji wenzake. Ana ubora wa ajabu na mapema au baadaye atauonesha kwani ni suala la muda tu."

Mbappe aliachwa nje ya kikosi cha Ufaransa kwa ajili ya mechi za kimataifa mapema mwezi huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hakuichezea nchi yake Oktoba huku kukiwa na wasiwasi kuhusu utimamu wa mwili, lakini kuachwa kwake kwa mara ya pili mfululizo kulikuja baada ya kutokosa mchezo wa klabu kwa takriban miezi miwili.

## Flick alia na kiwango Barca

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, alikosoa uchezaji wa timu yake baada ya viongozi hao wa LaLiga kuongoza kwa mabao mawili na baadaye kujikuta wakimaliza mchezo kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Celta Vigo pale kwenye dimba la Balaidos Jumamosi.



Mabao kutoka kwa Raphinha na Robert Lewandowski yaliwaweka Barca kwenye nafasi ya kuondoka na pointi tatu, lakini Celta walifunga mara mbili katika dakika sita za mwisho kupitia kwa Alfonso Gonzalez na Hugo Alvarez, na kupata pointi moja huku Marc Casado akitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Barca sasa hawajashinda katika mechi mbili wakiwa wamepoteza kwa Real Sociedad kabla ya mapumziko ya kimataifa na wameshindwa kushinda mechi yoyote kati ya tatu za ligi bila Lamine Yamal ambaye ni majeruhi.

„Wakati mwingine hutokea kwamba unaona uchezaji kama huu kutoka kwenye timu," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa kuelezea uchezaji wa timu yake.

„Sikutarajia kwamba tungecheza vibaya namna hiyo, lakini ndio hivyo. Tunapaswa kusimama na kusonga mbele. Ni mechi moja.

„Mwisho jambo bora zaidi ni kupata pointi moja. Ni jambo bora zaidi kuhusu leo, lakini hatuna furaha. Wachezaji hawana furaha, kila mtu hana furaha, na nadhani kila mtu anaweza kucheza vizuri zaidi kuliko leo (juzi)."

Licha ya kufungwa mabao 2-0, Celta ililingana na Barca kwa sehemu kubwa za mchezo na kusajili mikwaju sita zaidi ya lango kuliko wapinzani wao katika muda wote wa dakika 90.

## Arteta sasa amtetea Saka

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amemjibu mtu yeyote anayetilia shaka kujitolea kwa Bukayo Saka kwa kikosi cha England kwa kusisitiza kwamba „tutatuma vipimo vya MRI" kuthibitisha winga huyo alijeruhiwa wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa mwezi huu.

Saka alikuwa miongoni mwa wachezaji 10 waliojitoa katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Ugiriki na Jamhuri ya Ireland, hali ambayo nahodha Harry Kane alieleza kuwa „ya kukatisha tamaa."

Saka hakuweza kumaliza mchezo wa sare ya bao 1-1 wa Arsenal dhidi ya Chelsea kabla ya mapumziko ya kimataifa kutokana na tatizo la paja, lakini alicheza vema alipofunga bao la kuongoza katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi kwenye Uwanja wa Emirates.



Baadaye Thomas Partey na Ethan Nwaneri kila mmoja akafunga bao moja kukamilisha ushindi huo mnono, Arteta alitetea tofauti ya kutokuwapo kwa Saka England na kiwango kizuri akiwa Arsenal.

"Kweli, tunaweza kutuma vipimo vya MRI, ni rahisi sana," alisema Arteta. „Hayo ni mawasiliano ambayo yalikuwa wazi kati ya watu wa matibabu wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England.

"Hajafanya lolote, alikuwa hayupo na alihitaji muda wa kupona. Amefanya kikao kimoja cha mazoezi."

Arsenal walipata ushindi wao wa kwanza wa ligi tangu Oktoba 5, mwaka huu, na kutengeneza kasi nzuri kabla ya wiki ngumu inayoendelea na safari ya Jumanne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Sporting CP.

"Nilihisi nguvu kubwa katika saa 48 zilizopita," alisema Arteta.

"Jinsi kila mtu alivyorudi, nilihisi umoja mkubwa na nia ya kubadilisha hali na kile ambacho kimekuwa kipindi tofauti kwetu na hali zote ambazo tulilazimika kukutana nazo."

HABARI MICHEZO

## Ramovic aanika ubora wa Al Hilal

INATOKA UKURASA 24

mwaka 1988.

Yanga imeshinda mara mbili kati ya hizo kama ilivyo kwa Wasudan hao, huku zikitoka sare mara mbili pia. Mara ya mwisho timu hizo kukutana ilikuwa ni Oktoba 16, 2022 kwenye mechi ya raundi ya kwanza nchini Sudan, Al Hilal ikishinda bao 1-0 na kusonga mbele hatua ya makundi, baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Oktoba 8, mwaka 2022, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Kabla ya hapo, timu hizo zilikutana mara ya kwanza Januari 3, 1988, Al Hilal ikishinda mabao 2-0 katika hatua ya makundi ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati (Kagame Cup), na Januari 10, 1992, kwenye michuano hiyo hiyo, Yanga ilishinda kwa mikwaju 10-9 ya penalti katika mchezo wa nusu fainali baada ya suluhu ya dakika 90.

Kisha Yanga ikaenda kucheza fainali dhidi ya Simba, Zanzibar na kufungwa kwa mikwaju ya penalti, Mohamed Mwameja wakati huo aliyejiunga nayo akitokea Coastal Union, akiokoa mbili.

Mwaka 1994, mechi iliyochezwa Januari 7, Yanga na Al Hilal zilitoka sare ya bao 1-1 katika hatua za makundi, Kombe la Afrika Mashariki na kati, na Januari 10, 1999, Yanga iliichapa Al Hilal mabao 2-1 katika mchezo wa robo fainali.

## Fadlu awapa rungu Ateba ...

INATOKA UKURASA 24

kama ambavyo wamekuwa wakifanya siku zote na masuala ya ndani ya uwanja wawaachie wachezaji kwani watawalipa kwa ushindi.

"Mnachotakiwa ninyi ni kufika tu ili kuwapa hamasa wachezaji wetu. Pasi na kupepesa macho mechi ya Jumatano ni ngumu, kinachotakiwa ni kwenda kwa wingi ili kuwafanya wageni wajihisi kweli wapo ugenini, wanaweza kufungwa kwa makelele tu ya mashabiki.

"Bravo do Maquis ni timu ngeni na haina uzoefu sana wa mechi za kimataifa, ila ina wachezaji wazuri. Kwa sababu hawajawahi kuona umati wa mashabiki 60,000, siku wakikutana nao utawashangaza, utawatetemesha na kuwa faida kwetu.

"Kama timu kubwa mfano Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca, Raja Casablanca, Asec Mimosas na nyingine zinajua kasheshe la mashabiki wa Simba wakiwa Benjamin Mkapa," alisema.

Simba ipo Kundi A, na timu za Bravo do Maquis, CS Constantine ya Algeria na CS Sfaxien ya Tunisia.

# FEI TOTO AWASHTUKIA MAKIPA KUBAINI UPIGAJI PENALTI WAKE

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', amesema amewashtukia makipa wengi nchini kuwa wameshafahamu kuwa penalti zake huwa anapiga upande wao wa kulia, hivyo ameamua kubadilisha mwelekeo.

Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Tanzania, alitoa kauli hiyo juzi baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Azam na Kagera Sugar, akifunga bao pekee kwa mkwaju wa penalti, dakika ya 56, ikiiwezesha timu yake kushinda 1-0, mechi iliyochezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Fei Toto alisema mara nyingi penalti zake huwa anapiga upande wa kulia wa makipa, lakini ameshtuka baada ya kuona wengi wameanza kugundua hilo, hivyo akaanza mazoezi makali ya kubadilisha uelekeo na sasa anaweza kupiga upande wa kushoto kama alivyofanya kwenye mchezo huo na kumpoteza maboya kipa, Ramadhani Chalamanda.

"Makipa wengi wanajua mimi huwa napiga penalti upande wao wa kulia, nilipogundua hilo nikaanza mazoezi kwa ajili ya kupiga upande wao wa kushoto, kama ulivyoona kwenye mechi hii nimepiga upande nilioufanyia mazoezi na nimefunga," alisema Fei Toto.

Hilo linakuwa bao la pili kwa mchezaji huyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na yote akiyafunga kwa mikwaju ya penalti.

Oktoba 25, mwaka huu, kwenye uwanja huo, alifunga mkwaju wa penalti dakika ya 19, akiongoza timu yake kuiangamiza KenGold, mabao 4-1 katika moja ya michezo ya Ligi Kuu.

Ushindi huo unaifanya Azam kupanda mpaka nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikikaa juu ya Yanga ikiwa na pointi 24.

Azam na Yanga zote zina pointi 24 huku zikiwa zimefunga mabao 14 kila moja, lakini 'Wanalambalamba' wanakaa juu kutokana na kuruhusu idadi ndogo ya mabao, ikiwa imefungwa matatu, wakati Yanga ikiruhusu wavu wake kuguswa mara nne.

Azam imefikisha mechi ya 11, huku Yanga ikiwa haina mchezo wowote kutokana na mechi yao dhidi ya Fountain Gate kuahirishwa kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, hivyo imecheza mechi 10 tu mpaka sasa.

Kipigo hicho pia kinaifanya Kagera Sugar kusalia na pointi nane kwa michezo 11 iliyocheza ikiwa kwenye nafasi ya 14.

UMETUWEZESHA...




Wachezaji wa Timu ya Wanawake ya TP Mazembe, wakimrusha juu kocha wao, Lamia Boumehdi, baada ya kuwaongoza kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake kwa kuifunga AS FAR ya Morocco bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa nchini Morocco juzi. TP Mazembe ya DR Congo inakuwa klabu ya tatu kutwaa ubingwa huo baada ya Mamelodi Sundowns kuubeba mara mbili na AS FAR mara moja. Kwa kutwaa ubingwa huo imeondoka na Dola za Marekani 600,000 (Sh. bilioni 1.5 za Tanzania) huku AS FAR ikizawadiwa Dola 400,000 (Sh. bilioni moja) kwa kushika nafasi ya pili. **PICHA: MTANDAO**

# Kocha KVZ asifu safu ya kiungo Uhamiaji FC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya Maafande wa KVZ FC kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Wanajeshi wa Mipakani, Uhamiaji FC katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar wakati huu ikiwa mzunguko wa 12, wamekiri wapinzani wao hao kuwa bora zaidi katika eneo la kati.

Mchezo huo ambao ulipigwa juzi, Jumamosi katika dimba la Mau A majira ya saa kumi alasiri, ulivutia mashabiki wengi uwanjani hapo.

Kwa matokeo hayo KVZ FC imefikisha alama 21 ikiwa nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16 kama ilivyo ile ya Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha wa KVZ FC, Ali Khalid, alisema kupata ushindi huo mwembamba kumetokana na mchezo huo kuwa mgumu.

Alisema wapinzani wao waliwasumbua katika eneo la kati hali iliyosababisha kunyang'anywa mipira mara nyingi katika eneo hilo.

Khalid alisema wapinzani wao walikuwa bora katika eneo la kati na safu ya ulinzi hali iliyosababisha kushindwa kutumia nafasi walizotengeneza.

Alisema licha ya bahati kuwa kwao kwa kupakua ushindi huo, wachezaji wake walijituma bila kuchoka mpaka dakika za mwisho.

"Bado ligi ni ngumu sana, tumefanikiwa kupata alama tatu muhimu, licha ya ugumu wa mechi ambao unatokana na kuwa ukingoni mwa mzunguko huu wa kwanza kila mmoja mpango wake ni kushinda," alisema.

Hata hivyo, alisema wanajipanga kujikusanyia alama tatu katika michezo wao wa 13 wa ligi hiyo ili kujisogeza juu zaidi katika msimamo.

Michezo

Nipashe Jumatatu Novemba 25, 2024



Guardiola akiri maji ya shingo Man City

UKURASA 21



Afisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe (kushoto) na Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally (kulia jezi nyeupe), katika picha tofauti na nyakati tofauti wakihamasisha mashabiki jijini Dar es Salaam kununua tiketi kwa wingi kuelekea mechi zao za hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika zitakazopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho dhidi ya Al Hilal ya Sudan na keshokutwa dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola. **PICHA: WAPIGAPICHA WETU**

# Ramovic aanika ubora wa Al Hilal

## ●●● Atamba kuisoma vizuri na kuiandalia mkakati wa kuimaliza, rekodi zao zaonesha...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema amemaliza kazi ya kuisoma Al Hilal Omdurman ya Sudan na ameweka mipango kabambe namna ya kuikabili kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mechi ya raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

Akizungumza juzi jioni akiwa kwenye maandalizi ya kuelekea kwenye mchezo huo, alisema moja ya sifa ambayo ameiona kwao ni kwamba wako timamu kimwili na wanacheza vizuri, lakini hiyo haimaanishi hawafungiki, na ndiyo maana ametengeneza mipango kwa wachezaji wa safu ya ulinzi, viungo washambuliaji na mastraika jinsi gani ya kudili nao.

Alisema kwa kipindi kifupi ambacho amekabidhiwa timu hawezi kutengeneza kitu kikubwa, zaidi tu ya kuyaangalia makosa na ubora wa wapinzani wao na kuyafanyia kazi.

“Nimewaangalia Al Hilal namna wanavyocheza na najua nini watafanya, timu yao ni ngumu ipo timamu kimwili ila tayari nina mpango namna ya kucheza tunaendelea kufanyia mazoezi mbinu hiyo, nadhani kila kitu kitakaa sawa,“ alisema Ramovic.

Alisema kikosi chake kipo imara na ana imani wachezaji wake kufanyia kazi kile anachotoa kwenye mazoezi na kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa nyumbani wa Kundi A.

Alisema kazi kubwa aliyonayo ni kuwanoa mabeki wa Yanga wakiongozwa na Bakari Mwamnyeto, Yao Koussi, Dickson Job na Ibrahim Bacca, kuhakikisha wanafanikiwa kuwazuia washambuliaji wa Al Hilal, huku safu ya viungo washambuliaji, kina Clatous Chama, Stephane Aziz wakipeleka mipira mbele na kuwalisha mastraika, Clement Mzize na Prince Dube, ili kila idara ifanye inayokusudiwa kwa ajili ya kusaka ushindi wa kwanza.

Siku chache nyuma, Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, alisema ujio wa Ramovic kwenye kikosi cha Yanga umewachanganya kwani walikuwa wamejipanga kucheza kikosi cha mfumo wa Miguel Gamondi, lakini kuondoka kwake kumewaathiri kwa kuwa hawajui kocha huyo atacheza mfumo gani ingawa atalifanyia kazi hilo.

“Tulishamjua Gamondi aina yake ya uchezaji na mifumo, tulifanyia kazi namna timu yake inavyocheza, huyu mpya kwetu itakuwa ni mgumu sana, hatujui lolote, hatujui atakuja na mbinu gani. Tunatakiwa kuwa makini sana,“ alisema Ibenge.

Yanga itakutana na Al Hilal Omdurman ukiwa ni mchezo wa saba tangu timu hizo zilipokutana kwa mara ya kwanza

INAENDELEA UK. 23

# Fadlu awapa rungu Mukwala, Ateba kuiua Bravo do Maquis

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewapa kazi mastraika wake wawili, Leonel Ateba na Steven Mukwala, kuwamaliza Waangola, Bravo do Maquis, katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika, unaotarajiwa kuchezwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, kocha huyo raia wa Afrika Kusini, alisema kwa jinsi alivyowaangalia wapinzani wao, anadhani mastraika wake wana uwezo wa kuimaliza mechi hiyo kwa jinsi wanavyocheza.

"Malengo ni kupata ushindi nyumbani, ikiwezekana mkubwa tu, kwa kutumia nafasi tutakazotengeneza zitumiwe kwa usahihi na mastraika wetu ambao tumewapa kazi hiyo tu, kiufundi tayari tumeshawaangalia wapinzani wetu kwenye baadhi ya mechi, hasa ya Ijumaa, Novemba 22, waliyocheza dhidi ya Academica de Lobito kwenye Ligi Kuu nchini Angola,“ alisema.

Katika mchezo huo, Bravo do Maquis ikiwa ugenini ilitoka suluhu dhidi ya wenyeji wao.

Timu hiyo inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu nchini Angola ikiwa na pointi 16, ikicheza michezo 12, ikishinda mitatu, sare saba na kupoteza miwili, ikifunga jumla ya mabao 11, ikiruhusu 10 kwenye wavu wake.

"Mechi dhidi ya Pamba Jiji imetusaidia sana, imewafanya wachezaji wetu wawe kwenye utimamu wa mwili na tayari kwa mchezo huo mgumu, tofauti na tusingecheza, kilichotuathiri kwenye mechi ile ni hali ya uwanja na hali ya hewa, ndiyo maana hatukucheza vema, ila mashabiki wa soka wamiminike kuja kuona soka la kuvutia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa,“ alisema Fadlu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kuujaza uwanja

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >